

**Bibi** wa miaka 109 amwomba Rais Samia amsaidie kupata haki

UKURASA 3

**PM** kuongoza maziko ya Waziri Kwandikwa leo kijijini kwake Kahama

UKURASA 4




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Agosti 9, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580667

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Wahamasika chanjo corona

**ZITTO:** Ni salama, wananchi waichangamkie...

*Endelea ukurasa 2*




Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emanuel Tutuba (kushoto), akipeana mkono wa pongezi na Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Sabasaba Moshingi, baada ya uzinduzi wa Internet Banking katika benki hiyo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**UKURASA WA 3**

## WATAALAMU KUTHIBITISHA WAJAWAZITO, WANAONYONYESHA CHANJO UVIKO-19

WAJAWAZITO na wanawake wanaonyonyesha haijathibitishwa kama chanjo ya Uviko-19 ina madhara kwao mpaka itakapothibitishwa na wataalamu wa afya. Hayo yameelezwa na Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto, Mkoa wa Njombe...

**UKURASA 4**

## KORTI YATUPA RUFANI YA ALIYEMBAKA BINTI

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Tanga imetupilia mbali rufani iliyokatwa na Hassan Shabani aliyefungwa miaka 33 kwa kubaka na kumkata vidole binti baada ya kufanya kitendo hicho, kwa sababu haina msingi. Rufani hiyo ilitupwa...




Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na viongozi mbalimbali baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Dodoma akitokea Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## CHADEMA wamwombea Mbowe kanisani



UKURASA 2

## MUME, MKE WAJIUA MADAI YA WIVU WA KIMAPENZI

UKURASA 16

**MICHEZO** NABI KUAMUA HATIMA YA AMBUNDO, UKONDE UK. 23

**MAONI, KATUNI** UK.6

# CHADEMA wamwombea Mbowe kanisani

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

WANACHAMA na wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) mkoani Mwanza, wameendelea kufanya maombi kupitia makanisa mbalimbali kwa ajili ya kumwombea mwenyekiti wao, Freeman Mbowe, ambaye yupo gerezani kwa tuhuma za makosa ya ugaidi.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Epifania, Parokia ya Bugando, jijini Mwanza, Katibu wa CHADEMA Kanda ya Victoria, Zacharia Obad, alisema waliomba misa maalum katika kanisa hilo kwa ajili ya kumwombea mwenyekiti wao.

Alisema misa hiyo ilipata mwitikio mkubwa na wananchi wengi walishiriki wakiwamo wafuasi wa CHADEMA. Alisema nia yao ni kumwomba Mwenyezi Mungu aingilie kati kesi inayomkabili Mbowe ili haki itendeke.

"Mwenyezi Mungu awajalie Watanzania wote kupendana na kuhurumiana, hatuhitaji kuwa na chuki wala ugomvi katika kulijenga taifa letu, sisi sote ni Watanzania, tutaendelea kudai haki kwa njia ya amani ili tuweze kufikia lengo letu," alisema Zacharia na kuongeza:

"Katika kufanikisha hili tutaenda pia kwenye misikiti, kwa Wasabato na kwingineko ambako tutashiriki na Watanzania wenzetu katika kuitafuta haki kwa amani."

Alisema idadi ya wanachama waliojitokeza ni kubwa, kwani wapo walioungana nao, lakini hawakuvaa sare za chama, kwamba hatua hiyo inaonyesha ni kwa namna gani waliguswa.

Aidha, alisema kupitia matoleo katika misa hiyo, waumini wengi walivapongeza ikiwa ni ishara iliyoonyesha wapo pamoja nao na hawahitaji chuki wala masuala ya kubambikiana kesi, bali wanahitaji amani.

Aliwaomba Watanzania kuendelea kufuata miongozo ya kikatiba na kumwomba Mungu kupitia sala kwa imani zao na wanaamini watafanikiwa.

"Hata Paulo na Sila walikuwa gerezani wakamwomba Mungu na milango ikafunguka, na sisi tuna imani Mungu atawapa haki viongozi wetu Mama Samia na wenzake na watatenda haki," alisema Zacharia.

Katibu huyo alisema mwelekeo wa kuitafuta haki kwa njia ya amani kupitia makanisa ni mzuri kwani mwitikio wa waumini unaendelea kuongezeka, japokuwa wanachama wengine hawavai sare za chama wanaposhiriki ibada hizo.

Kadhalika, alisema viongozi wa dini wana nafasi kubwa ya kuamua mwelekeo wa nchi, ndiyo maana waliamua kutumia njia hiyo.

Ibada hiyo iliongozwa na Paroko wa Parokia hiyo, Padri Benedict, ambaye aliwapongeza na kuwashukuru wafuasi wa CHADEMA walioshiriki katika ibada hiyo.




Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel (katikati), akiongea na ujumbe kutoka nchini Saudi Arabia alipokutana nao jijini Dar es Salaam jana. Kushoto kwake ni Mkaguzi, Mamlaka ya Dawa na Chakula, Saudi Arabia, Ahmed Alhajouj. **PICHA: MBARAKA KAMBONA**

# Wahamasika chanjo corona

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imesema Watanzania 105,745 tayari wameshapatiwa chanjo ya UVIKO-19, huku 164,500 wakiwa wamejiandikisha kwa ajili ya kuchanjwa wiki hii.

Aidha, imeagiza vituo vyote vilivyoainisha kutoa chanjo hiyo kuwa wazi hata siku za mwisho wa juma.

Kwa mujibu wa taarifa kuhusu maendeleo ya usambazaji na utoaji wa chanjo hiyo iliyotolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Abel Makubi, uzinduzi wa utoaji chanjo mikoa yote ulikamilika Agosti 4, mwaka huu na tathmini inaonyesha kuwapo kwa mwitikio mkubwa wa wananchi.

"Rekodi ya makundi ya walengwa peke yake kufikia Agosti 7, mwaka 2021 ilionyesha zaidi ya 164,500 walikuwa wameshajiandikisha (booking) kwa ajili ya kupatiwa chanjo wiki hii, huku wengine 105,745 wakiwa tayari wameshapatiwa chanjo kufikia tarehe hiyo," alisema.

Aidha, alisema serikali inaendelea kuboresha huduma za upatikanaji wa vyeti kwa kukamilisha utaratibu wa kuhama kutoka kwenye mfumo wa vyeti vya makaratasi/vitabu na kwenda kwenye mfumo wa vyeti vya kidijitali (Covid 19 Vaccine Electronic Certificates).

"Hivyo, naomba kuwahakikishia wananchi kuwa taarifa zote za usajili na vyeti kwa wale waliochanjwa zimeandikwa katika vitabu na baadaye taarifa hizo zitahamishiwa katika mfumo wa ki-elekroniki," alisema Prof. Makubi.

Alitoa tahadhari iwapo kuna watu watakaojaribu kujipatia vyeti vya chanjo kwa njia za udanganyifu, kuwa watakaobainiwa na mfumo watachukuliwa hatua za kisheria.

"Ikumbukwe kuwa wizara inafahamu mfuatano wa namba zake na zimetolewa kituo gani, hivyo, ikitokea namba moja imejirudia uchunguzi utaanzia kwa watoa huduma waliotoa namba hizo na wateja wenye vyeti vya namba hizo," alisema.

Alitoa wito kwa watoa huduma ya chanjo na wapokea huduma kila mmoja kutimiza wajibu wake na kujiepusha na udanganyifu wowote.

"Kadi maalum za kielektroniki zinazoendelea kuandaliwa zitakuwa na vigezo vya kimataifa vya uthibitisho wa kupata chanjo ambapo vigezo hivyo ni pamoja na kuwa na utambulisho wa siri ambao utajumuisha taarifa za mpokeaji chanjo, chanjo aliyopata, muda na mahali alipopata chanjo husika."

"Kadi hizi zitatolewa kwa watu wote waliochanja hata wale ambao kwa sasa wamepewa cheti cha nakala ngumu nao watafikiwa ili kupewa cheti kipya ambacho kitasomeka kwenye mfumo wa kielektroniki," alisema.

Aliwaagiza watoa huduma kuwa kusiwapo na sababu yoyote ya walengwa wa chanjo kukosa au kukataliwa huduma.

"Kama ni suala la vitambulisho, basi serikali za mitaa zisaidie kuwatambulisha walengwa hawa hasa wazee wetu. Wizara inawaomba wananchi katika yale makundi yaliyoainishwa kupata chanjo kuendelea kujitokeza ili kutumia huduma hii," alisema.

Alisisitiza kuwa wizara hiyo inaendelea kuratibu utoaji wa chanjo hiyo kupitia vituo vya kutolea huduma za afya vya umma na binafsi vilivyoidhinishwa nchini.

**ZITTO ASEMA NI SALAMA**

Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema chanjo zilizoruhusiwa kuingizwa nchini ni salama.

Zitto alitoa kauli hiyo wakati akizungumza kwenye mkutano mkuu wa chama hicho uliokutana kwa dharura, jana Zanzibar.

"Napenda kuwahakikishia kuwa nimejiridhisha, chanjo zilizoruhusiwa kuingia nchini ni salama na mimi pia nimekwisha chanjwa na niko salama. Nipende kuwaasa kuwa chanjo ni suala la hiari, lakini tunapoangalia usalama wa wapendwa wetu, jamii yetu na Watanzania wenzetu basi hatuna budi kuhakikisha tunafanya maamuzi," alisema Zitto.

Alipongeza serikali kwa uamuzi sahihi wa kuruhusu chanjo ziingizwe nchini ili kuwapa kinga wananchi wake.

"Nimefarijika kwamba baada ya Rais Samia kuingia madarakani, kumekuwa na mwelekeo mpya wa kisera wa namna ya kukabiliana na janga hili la Uviko-19 nchini. Takwimu zimeanza kutolewa japo sio kwa ukamilifu na baadhi ya hatua za kujikinga zimeanza kuchukuliwa ingawa bado hatua hizi haziridhishi, lakini si haba, napenda kuipongeza serikali kwa maamuzi hayo sahihi," alisema Zitto.

"Napongeza maamuzi sahihi ya serikali kuruhusu chanjo ziingie nchini ili kuwapa kinga Watanzania na kulinda mfumo wetu wa afya dhidi ya wagonjwa wengi ambao bila kinga hawataweza kuhimili. Hata hivyo, bado kuna kazi ya kubwa ya kufanya kwenye uhamasishaji wa watu kujitokeza kupata chanjo."

Zitto alitoa rai kwa wanachama wa chama chake na wananchi kwa ujumla kufuata taratibu za kupata chanjo mapema.

Alishauri kuwapo na mkakati maalum wa uhamasishaji dhidi ya ugonjwa huo wa corona ambao utaongozwa na watu wanaoaminika kwenye jamii.

"Niweke bayana kwamba ni lazima kuwapo na mkakati maalum wa uhamasishaji dhidi ya corona ambao utaongozwa na watu wanaoaminika kwenye jamii."

■**Imeandaliwa na Agusta Njoji (Dodoma) na Elizabeth Zaya**

## HABARI KITAIFA

# Bibi wa miaka 109 amwomba Rais Samia amsaidie kupata haki

**Na Beatrice Shayo**

ALIYEKUWA Mkazi wa Kinondo 'A' Kata ya Mabwepande jijini Dar es Salaam, Dogo Hassan (109) (pichani), amemwomba Rais Samia Suluhu Hassan, kumsaidia kuingilia kati kesi yake ya mgogoro wa ardhi baada ya kuporwa ardhi yake akiwa mgonjwa na sasa hana mahala pa kuishi.

Kadhalika, amesema ucheleweshaji wa haki yake umesababisha watu kubomoa makaburi ya watoto wake pamoja na la mume wake na kujenga nyumba katika kiwanja hicho chenye ukubwa wa heka 10.

Akihojiwa na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, alisema kesi hiyo ilianza kusikilizwa mwaka 2016 na kupelekwa Baraza la Ardhi Kinondoni, mwaka 2018.

Alisema kesi hiyo imetumia muda mrefu hali iliyomsukuma kuomba msaada kwa Rais Samia ili aweze kumsaidia.

Alisema anaweza kufariki bila kupatiwa haki yake kwa sababu umri wake ni mzee na haoni hatima yake.

Akisimulia namna alivyoporwa ardhi yake alisema mwaka 1993 alifariki mume wake ambaye walikuwa wanaishi pamoja katika eneo la Kinondo 'A' Kata ya Mabwepande Tarafa ya Mji Mpya.

Alisema baada ya mume wake kufariki mwaka 1993 alianza kuugua ugonjwa wa kiharusi na kuchukuliwa na ndugu zake kwa ajili ya matibabu.

Anasimulia kuwa ugonjwa huo umemtesa katika kipindi cha miaka 15 na kuanza kurejea katika hali yake licha ya mguu wake mmoja na mkono haujaweza kunyooka vizuri.

"Wakati natibiwa walikuja watu wakavamia na kuanza kujenga katika eneo



langu ambalo wamenikuta naishi hapo tangu mwaka 1954 na watoto wangu tisa nimewalea katika hiyo ardhi," alilalamika.

Alisema jambo linalomuumiza ni ujenzi kuendelea licha ya kesi kuwa mahakamani.

"Nimekuwa wakutanga tanga mara kwa wajukuu mara kwa watoto naumia ninachotaka nirejeshewe ardhi yangu kabla sijafa," alisema.

Alisema awali alikuwa akifuatilia kesi hiyo katika Wilaya ya Kinondoni na kwamba kutokana na hali yake aliambiwa asiwe analetwa katika baraza hilo la ardhi kwa kuwa wanamchosha.

Alisema eneo hilo lenye ukubwa wa heka 10 limekuwa ni sehemu ya vita hata watoto wake wakienda wanataka kupigwa.

Mtoto wa bibi huyo, Mohamed Kinyuku, alisema baada ya kumchukua mama yao kwenda kumuuguza walimuacha dada yao mkubwa katika eneo.

"Hali ilivyozidi kuwa mbaya ilibidi dada yangu aondoke Kinondo 'A' na kuja kumuuguza mama wakati tunapambana na afya ya mama tukapatiwa taarifa kuna wavamizi wameingia katika ardhi yetu tukasema wacha tuendelee kumuuguza mama yetu kwa kuwa eneo lipo."

Alisema mama yao alipata nafuu mwaka 2015 na walianza kufuatilia eneo hilo na kupeleka kesi baraza la kata ilipokaa kwa muda mrefu aliomba barua kwa ajili ya kupeleka kesi mahakamani.

Alisema alipatiwa barua na kuifikisha mahakamani na waliitwa waliovamia.

Alisema kesi hiyo ipo tangu mwaka 2016 hadi mwaka huu haina uamuzi na hata wanapotaka kufika katika ardhi yao wanatishiwa kupigwa.

"Sasa mama yetu umri umeshamtupa wakati wowote Mwenyezi Mungu anaweza kumchukua tutapata wapi ushahidi katika lile eneo tumehangaika kupambania haki ya mama yetu tunakamwa," alisema.

"Tumeamua tuje kumuomba Rais na Waziri wa Ardhi aweze kumsaidia huyu mama apate haki yake bila hivyo sisi hatuna nguvu waliotuvamia wanatumia nguvu kubwa," alidai.

Alisema mama yake bado ana hali ngumu kwa kuwa hana makazi ya kuishi na afya yake hajatengemaa.

# Wataalamu kuthibitisha wajawazito, wanaonyonyesha chanjo Uviko-19

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAJAWAZITO na wanawake wanaonyonyesha haijathibitishwa kama chanjo ya Uviko-19 ina madhara kwao mpaka itapothibitishwa na wataalamu wa afya.

Hayo yameelezwa na Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto, Mkoa wa Njombe, Felisia Hyera, wakati akizungumza na Nipashe baada ya chanjo hiyo inayotolewa kituo cha Hospitali ya Rufani Mkoa wa Njombe.

Alisema kwa upande wa nchi bado haijathibitishwa makundi hayo kama wanaweza kuchanjwa au hawawezi.

"Kwa sasa hata waliopata hapa nchini bado hatujaingiza hilo kundi la wajawazito na wanawake wanaonyonyesha, japokuwa nchi nyingine wajawazito wamepewa, lakini kwa Tanzania bado hatujathibitisha," alisema Felisia.

Akizungumza baada ya kupata chanjo ya Uviko-19, Katibu wa Siasa na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Njombe, Erasto Ngole, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari Uviko-19 na kufuata ushauri wa wataalamu wa kupata chanjo ili waweze kuwa salama.

"Mimi tangu nazaliwa nina siku moja nilipata chanjo, chanjo ambayo nilipiga ilikua inatoka huko Ulaya, hatujawahi kutengeneza chanjo, dawa zote zinatoka Ulaya hata dawa za kufubaza Ukimwi zinatoka huko," alisema.

Alisema wimbi la tatu sio kitu kidogo, watu watoke wajumbani waje wachanjwe kwa usalama wao.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA**
**KILOSA S.L.P 29**
**KILOSA 01.07.2021**
**YAH: MAOMBI NA. 08/2021**
**DEVOTHA RAPHAEL NDOMBA ………… MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**ELIAS RAPHAEL NDOMBA ………………..,MJIBU MAOMBI**
**UDZUNGWA SACCOS LTD ……………………………..................**
**WITO/ KUITWA SHAURINI KWA ELIAS RAPHAEL NDOMBA**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Kilosa, Tarehe 12/08/2021 mwenyewe binafsi au mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kusikilizwa. Endapo hutahudhuria, Maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa maamuzi.

**Imesainiwa leo tarehe o1 mwezi 07 mwaka 2021**

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA(W)**
**KILOSA**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA / 84)**
**Mahakama ya Mwanzo ya KAWE**
**Wilaya ya KINONDONI**
**MADAI NAMBARI 106 YA 2021**
**Mdai HUSSEIN OMAR SALUM**
**Amdai**
**Mdaiwa MWANAHAWA SHILLA KILANGWA**
**Kwa: MWANAHAWA SHILLA KILANGWA – MBEYA**
**Kwa kuwa mdai / wadai ameleta / wameleta madai yake / yao kwamba / Eleza hapa habari ya madai**
**KUSIKILIZA KESI YA TALAKA NO. 106/2021**

Kwa hiyo unahitajika / mnahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMANNE tarehe 10/8/2021 saa 2:30 Asubuhi / Alasiri kwa kujibu madai haya. Na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wake / wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo. Angalia kama hukuhudhuria / hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea / mmepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa hati hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa / mmeshindwa.

**Hati hii yatolewa kwa amri yangu cha Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 06/08/2021.**



**KUPOTEA KWA KADI YA TREKTA**

**TANIEL JAPHET GOMAH** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA TREKTA AINA YA NEW HOLAND YENYE NAMBA ZA USAJILI **T843 BTC.** ENGINE NO **061743N.** CHASSIS NO **1161276.** KWA ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: ARU/ARU/ **RB /347533/2021.**



**The Guardian Limited**

**VACANCY**

**Freelance Sales Executives**

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales personnel to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Zanzibar, Tanga, Morogoro and Kilimanjaro.**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

**Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15th August, 2021.**

61637602

## Majambazi yavamia kwa mfanyabiashara

**Na Said Hamdani,** LINDI

KUNDI la watu wanaosadikiwa kuwa ni majambazi wamevamia nyumbani kwa mfanyabiashara Mustapha Gea (25), mkazi wa Kijiji cha Nduruka na kupora bidhaa mbalimbali, zikiwamo simu za mkononi, vocha, fedha taslimu na kutokomea nazo.

Taarifa kutoka kwa baadhi ya mashuhuda na wakazi wa kijiji hicho, wilayani Liwale ambazo pia zimethibitishwa na mamlaka husika, zinaeleza uhalifu huo ulifanyika Agosti 4, mwaka huu, saa 7:30 usiku.

Ni tukio la pili kufanyika mkoa wa Lindi ndani ya kipindi cha wiki moja. Tukio lingine lilifanyika Julai 30 baada ya watu wanaodaiwa kuwa majambazi kuvamia Kata ya Naipanga, Wilaya ya Nachingwea na kuingia nyumbani kwa wakala wa pesa, kujeruhi watu wawili na kupora simu, vocha, mkoba na fedha taslimu zaidi ya Sh. 5,240,000.

Kwa mujibu wa mashuhuda wa tukio hilo, kundi la watu wasiopungua saba, wakiwa na silaha za moto, walifika nyumbani kwa mfanyabiashara Gea na kuvunja mlango kwa kutumia jiwe maarufu kwa jina la 'Fatuma' na kuingia ndani.

Mashuhuda hao ambao hata hivyo hawakupenda majina yao yatajwe, walidai majambazi hayo baada ya kuvunja mlango walimweka chini ya ulinzi na kumuamuru kuwapatia kile walichokihitaji na kuondoka nacho.

Jitihada za mwandishi wa habari hizi kumpata mfanyabiashara huyo kuhusu tukio hilo hazikufanikiwa.

Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, ACP Mtatiro Kitinkwi, alithibitisha kutokea kwa uhalifu huo ambaye alisema majambazi hayo yalipora simu mbili, vocha, kadi za benki, vitambulisho vya kupigia kura na fedha taslimu, jumla ya Sh. 5,240,000.

Agosti 5, saa 7:30 usiku, watu wanne wanaosadikiwa ni majambazi wameuawa katika kurushiana risasi na askari polisi, eneo la makutano ya Barabara Nanganga Station kwenda Nachingwea, Ruangwa na Lindi na miili yao kuhifadhiwa Hospitali ya Mkoa Sokoine, mjini humo.




Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Ibrahimu Chiputula (wapili kushoto), akisoma hotuba ya kufungua mkutano wa Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo, mbele ya madiwani (hawapo pichani), kikao hicho cha robo ya nne kimefanyika jana mjini Masasi. Wengine ni Makamu Mwenyekiti wa Madiwani, Athony Chiako (kushoto), wapili kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Joshua Sanga. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Waziri Mkuu kuongoza maziko ya Kwandikwa leo

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, leo anatarajiwa kuongoza maziko ya aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Elias Kwandikwa, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga na kuongeza kuwa maandalizi ya maziko ya Kwandika yamekamilika.

Kiswaga alisema kuwa kaburi atakalozikwa Kwandika ambaye alikuwa Mbunge wa Jimbo la Ushetu limeshaandaliwa na askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ). Kiswaga aliwaeleza waandishi wa habari kuwa mwili wa Kwandikwa ulitarajiwa kuletwa jana mchana moja kwa moja Kijiji cha Butibu na kupokelewa na viongozi mbalimbali na wananchi.

Kuswaga alisema jana ingefanyika ibada fupi nyumbani kwake na leo kuzikwa katika eneo lililotengwa na familia kwa ajili ya maziko.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ushetu, Emanuel Makash, alisema walikaa kamati ndogo ambayo itaongoza shughuli za msiba kwa kushirikiana na kamati zingine zilizoundwa ili kufanikisha maziko hayo.

Mdogo wa Kwandikwa, Emily Kwandikwa, alisema ameungana na serikali na wananchi wengine kuhakikisha anatoa ushirikiano wa kumuhifadhi ndugu yake.

Baadhi ya wananchi wa Jimbo la Ushetu na maeneo ya mikoa ya jirani wameanza kuwasili katika Kijiji cha Butibu kwa ajili ya kushiriki kwenye maziko hayo.

Kwandikwa alifariki dunia Jumanne jijini Dar es Salaam na Ijumaa Rais Samia Suluhu Hassan aliongoza mazishi ya waziri huyo jijini Dar es Salaam.

# Korti yatupa rufani ya aliyembaka binti

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Tanga imetupilia mbali rufani iliyokatwa na Hassan Shabani aliyefungwa miaka 33 kwa kubaka na kumkata vidole binti baada ya kufanya kitendo hicho, kwa sababu haina msingi.

Rufani hiyo ilitupwa mbele ya Jaji, Dk. Ubena Agatho, baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili zilizokuwa zinapingana kutokana na hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Wilaya ya Muheza.

Mlalamikaji alishtakiwa katika Mahakama ya Muheza akikabiliwa na mashtaka mawili, shtaka la kwanza kubaka na shtaka la pili kujeruhi na kusababisha maumivu makali. Inadaiwa Aprili 4, mwaka 2019, katika Kijiji cha Mhamba wilayani Muheza, mlalamikaji anadaiwa kumbaka binti wa miaka 17 baada ya tukio hilo alimkata vidole vya mkono wa kushoto kwa kisu.

Upande wa Jamhuri katika kesi hiyo walileta mashahidi sita akiwamo daktari aliyemfanyia uchunguzi binti ambaye aliithibitishia mahakama kwamba binti aliingiliwa na vidole vyake vilikatwa na kitu kikali.

Mlalamikaji alikuwa na mashahidi watatu akiwamo mwenyewe, alipinga kuhusika katika tukio hilo na kudai kwamba alibambikiziwa kesi.

Alidai anaamini kesi hiyo ilitokana na mgogoro wa ardhi kati yake na shangazi yake, anadai kesi ilitengenezwa na mwenyekiti wa kijiji na shangazi yake huyo.

Mahakama ya Wilaya baada ya kusikiliza ushahidi wa binti ambaye alidai siku ya tukio mlalakaji alivaa bukta nyeusi, alikuwa kashika kisu na alimuona vizuri kabla ya tukio.

Mahakama hiyo ilisema upande wa Jamhuri umethibitisha mashtaka bila kuacha shaka, hivyo ilimtia hatiani mlalamikaji na kumpa adhabu ya kwenda jela miaka 30 kwa kubaka na miaka mitatu kwa kujeruhi.

Mlalamikaji alikata rufani akipinga adhabu hiyo akiwa na sababu nane, anadai mahakama ilikosea kuona Jamhuri imethibitisha makosa yake bila kuacha shaka.

Anadai hakimu hakuutilia maanani ushahidi wake wa utetezi na hakutoa sababu kwanini hakuuamini ushahidi huo.

Katika hoja zake alidai kesi hiyo ilitungwa kutokana na mgogoro wa ardhi kati yake na shangazi yake.

Anadai hayajui makosa hayo, lakini anaamini yaliundwa na Mwenyekiti wa Kijiji na shangazi yake kutokana na mgogoro wa ardhi.

Mahakama Kuu baada ya kusikiliza hoja pamoja na kupitia ushahidi ilikubaliana na hukumu ya Mahakama ya Wilaya ya Muheza iliyoona ushahidi wa mshtakiwa haukuwa na uzito ukilinganisha na ushahidi wa upande wa Jamhuri.

"Tuhuma kwamba kesi ilitengenezwa na Mwenyekiti wa kijiji na shangazi yake mlalamikaji ni hoja mpya, hazijawahi kutajwa wala kuungwa mkono na mashahidi wengine wa upande wa mlalamikaji," alisema Jaji Agatho.

Jaji Agatho alisema mahakama inaona rufani iliyopo mbele yake haina msingi, hivyo ilitupiliwa mbali.

HABARI KITAIFA

# 17 wafikishwa kortini madai kupokea rushwa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Morogoro imewafikisha mahakamani watuhumiwa 17 wa matukio ya kupokea rushwa, katika kipindi cha Aprili hadi Juni, mwaka huu.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Morogoro, Manyama Tungaraza, alisema hayo katika taarifa yake kwa umma juu ya utekelezaji wa kazi wa taasisi hiyo kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Aprili hadi Juni 2021.

Alisema kesi hizo 17 zimefunguliwa katika mahakama mbalimbali za wilaya zilizopo mkoani humo, kwamba kesi 10 zilitolewa hukumu na upande wa Jamhuri ilishinda kesi tisa na kushindwa moja.

Alisema kuna kesi ambazo zilifunguliwa kipindi cha nyuma na sasa zinaendelea kusikilizwa katika mahakama mbalimbali zilizopo mkoani humo.

Mkuu huyo wa TAKUKURU alisema licha ya kushughulikia kesi hizo lakini wanatarajia kufanya uchunguzi kuhusiana na ununuzi, usambazaji wa dawa na vifaa tiba katika zahanati, vituo vya afya na hospitali zilizopo mkoani humo.

Tungaraza alisema katika cha Julai hadi Septemba, 2021 TAKUKURU imeweka mikakati ya vipaumbele vitatu ambavyo ni kufanya uchunguzi kuhusiana na ununuzi na usambazaji wa dawa na vifaa tiba.

Alisema uchunguzi huo ni kubaini endapo kuna vitendo ama viashiria vya rushwa ili kuchukua hatua stahiki dhidi ya wale watakaobainika kujihusisha na vitendo hivyo.

Alisema TAKUKURU itaendelea na uchunguzi wa tuhuma zote zinazohusiana na migogoro ya ardhi hususani urasimishaji ardhi ambao unalalamikiwa na wananchi wengi katika Mkoa wa Morogoro.

# Zitto: Mchakato wa Katiba mpya uendelee

**Na Elizabeth Zaya**

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema chama hicho kinaona bado kuna umuhimu wa kuendeleza mchakato wa kutafuta Katiba mpya.

Zitto alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza kwenye mkutano mkuu wa chama hicho uliokutana kwa dharura Zanzibar.

"Rais aliahidi kukutana na viongozi wa vyama vya siasa, na kuhusu mchakato wa Katiba mpya, aliomba apewe muda ili asimamishe uchumi. Wakati tukisubiri ahadi hiyo ya wadau wa siasa kukutana na uongozi wa serikali, bado uongozi wa chama chetu unaona ipo haja ya uwapo wa mchakato wa Katiba mpya, maana ni mchakato huo ndio utakaotusaidia kwa kina katika hiyo kazi ya kujenga uchumi," alisema Zitto.

"Katika kipindi hiki, taifa letu linatakiwa kuwa moja na sio kuwa vipande vipande, hakuna sababu ya kugawanyika kwa sababu ya Katiba ambayo mchakato wake ulishaanza na Rais Samia ndiye alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba. Nipendekeze kuwa wadau wa siasa tutake na kukubaliana namna bora ya kufikia malengo ya kuwa na Katiba mpya."

"Kupitia mazungumzo ya vyama vya siasa, hakuna kitakachoshindikana, ni lazima tuanze kujenga utamaduni wa kusikilizana na kukubaliana au hata kukubaliana lakini lazima tukaekwanza. Haitakuwa na maana kuendelea kujenga nchi wakati taifa linaporomoka."

Zitto aliipongeza serikali ya awamu ya sita kwa kurudisha uhuru wa vyombo vya habari, kuondoa ukusanyaji wa kodi kandamizi, kufuta baadhi ya kesi.

"Serikali mpya imefanya mambo kadhaa tangu iingie madarakani ambayo ni kinyume na yale yaliyomomonyoa umoja wa kitaifa miaka mitano na nusu iliyopita, hatua hizi si haba, lakini kwa uharibifu uliofanyika si hatua za kutosha," alisema Zitto.

Zitto alisema jambo kubwa katika nyanja ya siasa ambalo bado serikali haijafanya ni uhuru wa kisiasa.

"Kwetu tuliopo kwenye siasa, jambo kubwa ambalo serikali mpya ya Jamhuri haijalifanya vizuri ni uhuru wa kisiasa. Bado sheria ya vyama vya siasa ni ya mwaka 2019, bado sheria za uchaguzi ni zile zile na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ni ile ile na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ni ile ile."

"Ni rai yangu na viongozi wenzangu tuwe na majadiliano ya kitaifa ili kwanza kuganga yaliyopita na kukubaliana namna ya kwenda mbele katika kujenga upya demokrasia yetu. Ninamsihi Rais Samia kuweka mazungumzo haya kama kipaumbele kikubwa cha kuponya taifa na kuleta nchi pamoja."

Akizungumzia kuhusu suala la Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, Zitto alimwomba Rais Samia kuingilia kati suala linalomkabili kiongozi huyo wa upinzani nchini.

"Jambo hili la mashtaka dhidi ya Freeman Mbowe linaondoa uwezekano wa murua wa kuwa na majadiliano mema ya kisiasa nchini, ni jambo linalokumbusha machungu makubwa sana, ni jambo linaloipasua zaidi nchi, ni jambo linalochochea zaidi chuki, ni jambo ambalo tukiliacha na tusilipinge basi litaondoa kabisa fursa iliyopo mbele yetu ya kuanza upya," alisema Zitto.

"Litazidisha chuki kubwa ya kisiasa iliyoko, na itavunja imani, matumaini na matarajio kiasi ambayo yaliwekwa kwa serikali hii mpya. Wito wangu kwa Rais, ni kuingilia kati na kumaliza jambo hili la kisiasa kwa njia za kisiasa."

"Ninaomba Rais Samia aingilie jambo hili na kuhakikisha Mbowe anaachiwa huru na mashtaka dhidi yake yanafutwa kabla mambo hayajaharibika zaidi. Ni nasaha zangu pia viongozi na wanachama wengine wa vyama vya siasa na wanasiasa waliokamatwa kwa makosa yanayotokana na shughuli za kisiasa waachiwe huru ikiwamo wananchi wengine wanaosota mahabusu kwa miaka kadhaa."



Mjasiriamali akiwa amebeba vinu vya kutwangia akitafuta wateja katika eneo la Banana jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Operesheni EWURA kusaka wauza gesi wadanganyifu

**Na Richard Makore,** MWANZA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetangaza kuanza kufanya msako kwa wafanyabiashara wa gesi za majumbani wanaouza mitungi ambayo haijatimia ujazo.

Kadhalika, imewaomba wananchi ambao wanatumia nishati hiyo kutoa taarifa kwao pindi wanapohisi wameibiwa kwa kuuziwa mitungi ya gesi ambayo haijatimia ujazo wake.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake jana jijini Mwanza, Meneja wa EWURA, Kanda ya Ziwa, George Mhina, alisema wamebaini baadhi wa wafanyabiashara wakubwa wa gesi kudanganya kuhusu ujazo wa mitungi hiyo.

Alisema sheria ya EWURA inawataka kuwapa onyo wafanyabiashara hao wasiokuwa waaminifu ama kuwatoza faini na adhabu ya mwisho ni kuwafutia leseni zao.

Aliongeza kuwa kuna mitungi ya kilo tano na kilo 15 ambayo mara nyingine hutumiwa na wananchi majumbani, lakini baadhi yake uzito wake hautimii.

"Unakuta baadhi ya wafanyabiashara wanajaza gesi kwenye mitungi kiholela na hiyo inachangia kutotimia uzito wake lakini pia ni hatari sana kwa usalama wa wananchi kwa kuwa inaweza kulipuka," alisema Mhina.

Mhina alisema kwa sasa kuna mwamko mkubwa wa watu kutumia gesi majumbani kuliko nishati nyinginezo hususani maeneo ya mijini.

Aidha, alisema sehemu za vijijini licha ya kutumia mkaa na kuni ambavyo siyo rafiki wa mazingira, lakini na wao wameanza kutumia gesi ambayo inatunza mazingira.

Meneja huyo alisema kwa sasa matumizi ya gesi hapa nchini yanafikia tani 160,000, kwamba msako wanaotarajia kuufanya kuanzia wiki ijayo utawabaini wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu.

Kuhusu wananchi kutoa taarifa kwao wanapohisi kuibiwa, Mhina aliwaomba kufika ofisini kwao ama kuwapigia simu ili kutoa taarifa za uhalifu huo.

Kadhalika, Mhina alisema wanatarajia kuanza kufanya msako ili kuwakamata watu wanaouza mafuta ya petroli na dizeli barabarani kwenye chupa za maji.

Alisema biashara hiyo ya kuuza mafuta bila utaratibu imekithiri katika maeneo mbalimbali ya kanda ya ziwa, kwamba watahakikisha wanaikomesha ili kulinda usalama wa wananchi na mali zao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uchaguzi TFF umepita, sasa tushirikiane kuinua soka letu

**HATIMAYE** juzi, Jumamosi wajumbe wa mkutano mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), wametimiza wajibu wao kisheria kuchagua viongozi wapya watakaobeba dhamana ya kusimamia na kuongoza mpira wa miguu nchini kwa kipindi kingine cha miaka minne.

Katika uchaguzi huo uliofanyika jijini Tanga, Rais aliyemaliza muda wake, Wallace Karia, alifanikiwa kutetea kiti chake huku kwa mujibu wa Katiba ya TFF, Karia alitangaza wajumbe wanne wa kuteuliwa ambao ni Athumani Nyamlani, Ahmed Mgoyi, Saidi Soud na Hawa Mniga, aliyekuwa mgombea pekee mwanamke katika nafasi ya urais kwenye uchaguzi huo, lakini akaondolewa hatua za awali kwa kutokidhi vigezo.

Aidha, kwa mujibu wa katiba pia Karia alimteua Nyamlani kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa shirikisho hilo, na wajumbe wa mkutano mkuu walimthibitisha pasi na shaka kuendelea kukalia kiti hicho.

Wajumbe wengine waliokuwa wakigombea nafasi sita za Kamati ya Utendaji na kuibuka washindi ni Lameck Nyambaya, Khalid Abdallah, James Mhagama, Mohammed Aden, Vedastus Lufano na Issa Bukuku.

Kwa ujumla hilo ndilo jopo la uongozi mpya litakalobeba dhamana ya kufanya maamuzi ya mwisho katika soka letu, hivyo ni wakati sasa wakuweka tofauti zetu kando za kidini, kisiasa, kiitikadi, lakini kuvuja makundi yote ya kampeni ili kuwa kitu kimoja.

Nipashe tunaamini ushirikiano kwa viongozi na wadau wote wa soka pamoja na Watanzania kwa ujumla, ndiyo silaha pekee itakayoliwezesha soka la Tanzania kupiga hatua mbele zaidi na kuwa na ligi yenye ushindani mkubwa na kuifanya kupanda kutoka nafasi ya nane ambayo inashika kwa sasa katika viwango vya ubora barani Afrika.

Lakini pia tunaamini wote waliogombea nafasi mbalimbali tangu mwanzo wa mchakato wa uchaguzi huo ulipotangazwa Juni 8, mwaka huu hadi waliokosa kura za kutosha juzi, kwetu sisi wote ni washindi na mchango wao wa maoni ama mawazo ni muhimu sana katika kulisukuma mbele gurudumu la soka letu. Hatutarajii kuona makundi ama viongozi waliopitishwa na mkutano mkuu wakikosa ushirikiano kutoka pande yoyote ile, na watakaofanya hivyo kwetu daima ni wasaliti katika maendeleo ya soka na hawana budi kupigwa vita vikali.

Tunaamini Karia, Nyamlani pamoja na wajumbe wa Kamati ya Utendaji pekee, hawawezi kutosha kuliongoza soka pasipo kupata ushirikiano wa wadau wote wa soka na Watanzania kwa ujumla ili kuweza kufikia malengo yao ya kuona Tanzania inakuwa moja ya nchi zilizopiga hatua kubwa kisoka duniani.


Licha ya kutambua hakuna binadamu aliyekamilika, lakini busara na hekima zinapaswa kuchukua hatua zaidi pindi tunapowasilisha maoni na mawazo yetu pale tunapoona viongozi hao wameteleza katika kufanya maamuzi mbalimbali.

Pamoja na hayo neno letu kwa viongozi waliochaguliwa na kuteuliwa, hawana budi kutambua cheo ni dhamana, hivyo kutenda haki na si kutenda tu bali pia tunataka kuona haki ikitendeka kwa sheria na kanuni zilizopitishwa kwa maslahi mapana kwa wote.

Kadhalika, ili kuhakikisha viongozi hao wanatekeleza wajibu wao ipasavyo, ni wakati sasa wa wanachama wote wa TFF, klabu na wadau wao wote kufuata na kutii sheria na kanuni walizojiwekea kwani kwa kufanya hivyo kutaondoa manung'uniko yasiyo ya lazima.

Nipashe tunawataki kila kheri viongozi wote waliochaguliwa na kuteuliwa katika kuanza kutekeleza majukumu yao na mafanikio makubwa kwa kuhakikisha soka la Tanzania linapiga hatua zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanasimba wampa darasa Manara

Na Adam Fungamwango

**KATIKA** pitapita zangu nikakutana na mzee mmoja akaniita na nikaenda kumsikiliza ni kipi anataka kuniambia. Sikuwa namtambua na katika kumbukumbu zangu zijawahi kumuona hata siku moja. Alikuwa na umri mkubwa sana. Alikuwa anakamata bakora au mkongojo ambao ulikuwa unamsaidia kutembea.

Akasogea pembeni na kuashiria kutaka kuzungumza na mimi, nilimsogelea ili nimsikilize vizuri zaidi. Baada ya salamu akaniambia kuwa ameambiwa na watu kuwa mimi ni mtu wa habari. Nikamjibu ndiyo. Akatabasamu. Aliongea maneno ya hapa na pale ya kujitambulisha kuwa yeye ni mwanachama wa klabu ya Simba, ingawa ana miaka zaidi ya 30 sasa hajawahi kugusa kwenye klabu.

Akaniambia yeye si mwanachama tu, bali alishawahi kuichezea klabu ya Simba wakati huo ikiitwa Sunderland, akikipiga beki wa kushoto.

"Usinione hivi kijana, mimi nilikuwa nacheza beki wa kushoto vizuri sana, na ikasababisha hata nikapata kazi bandarini kwa mpira huu huu, na ukafanya nikajenga nyumba zangu tatu moja Mwananyamala nyingine Kinondoni na moja ipo Mburahati. Isingekuwa mpira na kuichezea Sunderland inaweze-kana nisingezipata, sasa nimestaafu, lakini naiheshimu sana klabu yangu ya Simba kwa sababu imenifanya niwe hivi nilivyo sasa, naheshimika," anasema mzee huyo ambaye aliniambia haina haja ya kumtaja jina, ila alichotaka yeye aeleze kinachomkera cha baadhi ya watu wakipata nafasi ya kuwa kwenye klabu hiyo wanataka kujifanya wako juu ya klabu.

"Nimemsikia aliyekuwa msemaji wetu eti akisema ameifanyia mambo mengi Simba na yeye amesababisha imejulikana zaidi na mchango wake utambuliwe, hivi kweli kila mmoja akitaka mchango wake utambuliwe Simba si itakuwa vurugu pale," anasema mzee huyo kwa ukali kidogo. "Mimi unavyoniona mbali na kucheza, nimejenga ile klabu, nimepandisha zege pale tena kwa kujitolea, mbona sijaenda kulalamika kuwa nimeifanyia mengi na mchango wangu utambuliwe?" Anahoji mzee huyo.

Alikuwa akisema hayo, kutokana na hivi karibuni Haji Manara, aliyekuwa Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya klabu ya Simba, mbali na mambo mengine, alidai kuwa ameifanyia mema mengi klabu hiyo na mchango wake uthaminiwe.

"Mimi na wanachama wenzangu tulikuwa tunatandika kitambaa chini pale Msimbazi, akipita mpenzi na shabiki tunawaomba watoe shilingi moja kwa ajili ya ujenzi, kwa hiyo mbali na vyanzo vingine, lakini watu wengi wamechanga pale. Siku ya kumwaga zege walikuja wanachama na mashabiki wengine tukapandisha zege juu bure bila kulipwa hata senti moja, na hii ni kwa mapenzi yetu. Tena siku hiyo ilikuwa mwezi wa toba, tulikuwa tumefunga, lakini tulifanya kazi hiyo kwa kuipenda tu klabu yetu. Hivi na sisi tuliojenga nao tuanze kupiga kelele? Ukifanya kitu kwa mapenzi yako, basi yaendeleze kuwa mapenzi tu, huwezi baadaye ukalalamika, hizi klabu wanachama na mashabiki wanajitolea tu, hawawekezi kupata faida baadaye. Kuna watu mimi nawaona mwaka mzima wanasafiri na timu kuishangilia kila mkoa timu inakokwenda, wale nao pia wana mchango si yeye peke yake."

Mzee huyo anasema Manara alichotakiwa kudai ni malipo yake kama yapo kwa mujibu wa sheria, lakini si kusema ndiyo ameipandisha chati Simba.

"Simba inajulikana tangu wakati wa Sunderland bwana, wakati sisi tunacheza mbona wenyewe hatusemi tumeifikisha hapo ilipo?" Maneno ya mzee huyo yanawakilisha wengi ambao walikuwa wanalifuatilia sakata hilo, baada ya Manara kuandika barua ya kuacha kazi na klabu ya Simba kuafikiana nayo, ikimteua Ezekiel Kamwaga kuwa Kaimu Ofisa habari wa klabu hiyo.

Ni kweli, inawezekana Manara alikuwa chachu ya baadhi ya vijana wa kisasa kushabikia Simba, lakini haiwezi kuwa ndiyo iwe sababu ya kutokuwa na nidhamu kwenye klabu na kujiona mkubwa kuliko mwingine. Simba ni taasisi ambayo kila mmoja ana mchango wake. Kila mmoja anaweza kuwa ana mchango wa kuingiza baadhi ya mashabiki.

Unaweza ukakuta wapo baadhi ya mashabiki wa klabu hiyo waliipenda kwa sababu ya Abdallah Kibadeni alipokuwa anacheza, au Mohamed Mwameja, Juma Kaseja, Nteze John, Zamoyoni Mogella, Hamisi Gaga, Aishi Manula, Meddie Kagere, Clatous Chama na wengine wengi. Lakini hakuna hata mmoja anayeweza kujigamba au kujiona mkubwa kuliko taasisi yenyewe. Klabu ya Simba ilianzishwa mwaka 1935 na imeendelea kuwapo hadi leo, ikipitia viongozi mbalimbali na wachezaji wengi tu. Hao wote wana mchango wa kuifikisha hapa na si mtu mmoja aibuke leo na kusema ameifanya klabu kuwa maarufu.

Watu watakuja, wataingia Simba, watatoka, vitakuja vizazi vingine klabu itabaki pale pale kama ambavyo viongozi wa sasa wameirithi kutoka kwa waliopita. "Manara anatakiwa akumbuke tu kuwa hata umaarufu wake umetokana na kuwa kwenye klabu hiyo. Sidhani kama angekuwa alivyo kama angekuwa kwenye klabu kama Ihefu FC.

"Ndiyo maana nayakumbuka maneno ya Mwekezaji wa Klabu ya Simba, Mohamed "Mo" Dewji, siku ambayo anaingiza kwenye akaunti pesa za uwekezaji kiasi cha bilioni 20 kuwa "Simba ni kubwa kuliko mtu."

Ni kweli ni hatari kuwa na mtu ambaye tayari alishaonekana au kujiona ni mkubwa kuliko taasisi ambayo imemfanya awe hapo alipo. Kwa sababu atakachofanya ni kutaka kuishusha taasisi akidhani yeye atabaki kuwa juu yake.

## HABARI KITAIFA

# Ukatili wa kijinsia washtua madiwani

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MATUKIO ya ukatili wa kijinsia wilayani Njombe yakiwamo mimba za utotoni yametajwa kuongezeka kwa kasi, huku madiwani wakitaka hatua zichukuliwe.

Wanafunzi 34 wa shule za msingi na sekondari Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wamekosa masomo, kwa sababu ya kupata mimba wakiwa shuleni kwa kipindi cha mwaka 2020 na 2021.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Avelino Chaula, alibainisha hayo wakati akitoa elimu kabla ya mkutano wa Baraza la Madiwani, ambapo alisema kwa mwaka 2020 wanafunzi 16 walipata kati yao mmoja ni wa shule ya msingi na mwaka 2021 wanafunzi 18.

"Licha ya matukio ya mimba, kwa kipindi cha miaka miwili tuna matukio 161 ya ukatili wa kijinsia, lakini matukio yanayoongoza kwa wingi ni ya utelekezaji na ukiangalia matukio ya utelekezaji kwa mwaka wa kwanza tuna matukio 42, na mwaka wa fedha 2020, 2021 tuna matukio 57 na haya ni kwa yale yaliyotufikia ofisini sasa tujiulize ni mangapi hayajafika?' Alihoji na kuwaomba wazazi wawajibike kulea watoto.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya madiwani, Neema Mbanga, Isaya Myamba na Roida Wandelage, walitaka kuwekwa kwa mikakati maalum ya kushughulikia changamoto za ukatili ikiwamo tatizo la kesi nyingi za ujauzito wa watoto kutomalizika.

"Watoto wengi wanapita mimba, lakini ukianza kufuatilia unaona tu imeishia hewani kwa hiyo ninaomba halmashauri muwe makini na kuyafuatilia haya kwa nguvu zote," alisema Neema.


"Nadhani kuna sababu ya msingi ya kujipanga upya namna ya kudhibiti na kushughulikia kesi hizi kuhakikisha zinaisha," alisema Myamba.

Naye Roida Wandelage alisema: "Mtaani kuna kawaida ya kusema kipi bora nimfunge yule ambaye amempa mtoto mimba au nimuache anilelee mtoto wangu na haya wanayafahamu."

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, George Makacha na Valentino Hongoli, Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, waliwataka madiwani na maofisa watendaji kuitumia mikutano yao ya hadhara kuhakikisha wanatoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia katika jamii pamoja na mimba za utotoni.

"Sheria inataka kama mtoto amepewa mimba lazima sheria zichukuliwe na sisi kama viongozi ni vema tutoe elimu zaidi ili wazazi waelimike na kuona uchungu juu ya watoto," alisema Makacha.

Hongoli alisema: "Wakati mwingine sisi wenyewe tukijitathmini utakuta viongozi, watendaji na baadhi ya wananchi wanaonekana kioo kwenye jamii, lakini utakuta ni watelekezaji wa watoto."




Kaimu Meneja wa Mgodi wa Barrick Bulyahulu, Dk. Zumbi Musiba (kulia), akikabidhi hundi ya Sh. milioni 300 ya malipo ya ushuru wa huduma kwa Mkuu wa Wilaya ya Nyang'hwale, Jamhuri David William (kushoto), katika hafla iliyofanyika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaja na mikakati uboreshaji sekta ya uvuvi

**Na Maulid Mmbaga**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah, amesema serikali imejipanga kwa kuweka mikakati ya kimaendeleo kwa miaka mitano, ambayo imetoa kipaumbele katika suala la uwekezaji.

Dk. Tamatamah aliiambia Nipashe kuwa maeneo makubwa ambayo yamelengwa katika uwekezaji ni uwekezaji wa uvuvi katika bahari kuu, ambao katika miaka mitano ijayo kwa upande wa bara serikali itanunua meli tano.

Alisema katika mwaka unaokuja, serikali itanunua meli tatu kati ya tano zilizopo ndani ya mpango, na zitakuwa zinaendeshwa na Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) kwa kushirikiana na sekta binafsi.

"Sambamba na hilo uwekezaji mwingine mkubwa ambao serikali itaufanya ni ujenzi wa bandari ya uvuvi Bagamoyo, taratibu za maandalizi zimeshaanza, na tunategemea mwezi wa 10 tutaanza kutangaza zabuni ili ujenzi uanze," alisema.

Aliongeza kuwa kwa kuanzia, serikali imetenga shilingi bilioni 50 zitakazotumika kuanza ujenzi huo, na kwamba ujenzi huo utakuwa na manufaa mengi ikiwamo kuongeza kiwango cha uvuvi wa samaki.

Alisema faida nyingine ni kusaidia malighafi katika viwanda vya ndani pamoja na kusaidia wafanyabiashara kwa kupata samaki kwa bei nzuri.

"Eneo lingine la kuhakikisha tunaongeza uzalishaji wa samaki ni kupitia ufugaji au ukuzaji viumbe maji, watu wamehamasika katika ufugaji wa samaki... mwaka jana tulikuwa na wafugaji zaidi ya 20,000, na baada ya mwaka mmoja wameongezeka na kufikia 30,000," alisema.

Aidha, kila wanavyoongezeka watu ndipo mahitaji ya vifaranga vya samaki na chakula bora vinaongezeka, pia katika mwaka huu wanategemea uzalishaji utaongezeka kutoka tani 20,000 hadi tani 30,000, na kufikia mwaka 2030 wanategemea kufikia uzalishaji wa tani 100,000 za samaki.

# Mifuko 200 ya saruji yadaiwa kuharibika kusubiri maelekezo

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAKATI serikali ikihimiza ujenzi wa vyumba vya madarasa, mifuko 200 ya saruji yenye thamani ya zaidi ya Sh. 3,000,000 iliyopelekwa kujenga madarasa Sekondari Kata ya Nangaru, Manispaa ya Lindi, imeanza kuharibika kwa madai ya kusubiri maelekezo kutoka kwa uongozi.

Diwani wa Kata hiyo, Salum Bakari Ng'ondo, alisema hayo kwenye kikao cha Baraza la Madiwani, kilichofanyika mjini humo.

Ng'ondo alitaka kufahamishwa sababu zinazokwamisha kutotumika vifaa vya ujenzi vilivyopelekwa kwenye kata yake, ikiwamo saruji iliyopelekwa miezi saba iliyopita ambayo alidai imeanza kuharibika (kuganda).

"Naomba kupewa majibu leo hii simenti tuliyoletewa tayari imeanza kuganda, sababu za ucheleweshwaji huu nini?" Alihoji.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Lindi, Baptista Kianza, akitoa ufafanuzi, alitaja kinachokwamisha ni pamoja na kutompata kwa haraka mzabuni wa kupeleka matofali kwenye kata hiyo, kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa vyumba hivyo kwa shule hiyo.

Pia Kianza ambaye ni Ofisa Utumishi wa Manispaa hiyo, alisema kutokana na kuchelewa kumpata mzabuni wa kupeleka matofali katika kata hiyo, ni vyema saruji hiyo ikatumika kwa kazi nyingine ya kimaendeleo ili kuokoa iliyobaki isiendelee kuharibika.

Diwani Ng'ondo akizungumza na mwandishi wa habari hizi baada ya kikao hicho, alisema saruji mifuko 300 na vifaa vingine zikiwamo ndoo za rangi, zimepelekwa mwezi Januari mwaka huu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na vyoo kwa sekondari ya kata yao.

Alisema kati ya idadi hiyo ya saruji ni mifuko 100 pekee iliyotumika, huku 200 ikiendelea kuganda kusubiri maelekezo mengine kutoka kwa uongozi wa Manispaa ya Lindi.

# Tanzania yasaka soko la nyama Saudi Arabia

**Na Mbaraka Kambona**

TANZANIA inaendelea kufanya jitihada za kutafuta soko la nyama nchini Saudi Arabia.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa maekelezo yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuitaka kutafita soko la nje kwa ajili ya bidhaa hiyo.

Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel, alibainisha hayo baada ya kukutana na kufanya mazungumzo na ujumbe kutoka Saudi Arabia, kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara ya nyama na nchi hiyo.

Prof. Ole Gabriel alikutana na ujumbe huo ulioongozwa na Mkaguzi, Mamlaka ya Dawa na Chakula, Saudi Arabia, Ahmed Alhajouj, jijini Dar es Salaam juzi.

Kwa mujibu wa Prof. Gabriel, kabla ya kukutana nao, ujumbe huo ulipata fursa ya kutembelea na kuona maeneo mbalimbali yanayohusika na uchakataji wa mazao ya mifugo ikiwamo machinjio, maabara na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ambapo kote walijiridhisha na kutoa mapendekezo kadhaa ya kuboresha ili biashara hiyo iweze kufanyika kwa viwango vinavyotakiwa na nchi hiyo.

Alisema kuwa Rais Samia Suluhu ameielekeza wizara hiyo kutafuta masoko nje ya nchi, hivyo wizara inaendelea kufanya jitihada ikiwamo hatua hiyo ya kutafuta soko Saudi Arabia.

"Haya masoko ya nje ya nchi ni mazuri kwa sababu yanatupatia fedha za kigeni, lakini pia yanawahakikishia wafugaji wetu soko la uhakika kwa mazao ya mifugo yao," alisema Prof. Ole Gabriel. Prof. Gabriel alitoa rai kwa wafugaji nchini kuchukulia hatua hiyo kama ni fursa kubwa, hivyo wahakikishe wanaboresha ufugaji wao kuwa wa kisasa zaidi ili kukidhi soko la kimataifa.

"Serikali ni rahisi kutafuta masoko, lakini je, mifugo iliyopo inakidhi soko hilo?" Alihoji na kuwaomba wafugaji na wafanyabiashara watumie fursa hii vizuri ili kuboresha uchumi wao na wa Taifa.

Alisema Sekta ya Mifugo kwa sasa inachangia katika pato la Taifa kwa asilimia 7.4, ingawa lakini lengo la Wizara ni kufikia asilimia 15 ifikapo mwaka 2025, na kwamba hilo linawezekana kama milango ya masoko nje ya nchi ikianza kufunguka kwa uhakika.

Prof. Ole Gabriel aliongeza kuwa wizara itatoa ushirikiano kwa kila mdau anayechangia katika mnyororo wa thamani wa mazao ya mifugo kuhakikisha kunakuwa na mazao bora kwa ajili ya soko la ndani na la nje.

Naye Msajili wa Bodi ya Nyama, Dk. Daniel Mushi, alishukuru serikali kwa jitihada inazozifanya kwa kushirikiana na wadau kufungua masoko mengine nje ya nchi ili kuuza nyama katika masoko yanayolipa bei nzuri.

Aliongeza kuwa ujio wa ujumbe huo umewapa changamoto, kwani kuna mambo wanapaswa kufanya ili nyama ya Tanzania iweze kukubalika katika masoko ya nje.

Aliendelea kusema kuwa ili kufikia masoko hayo ni lazima kuboresha lishe ya mifugo ili wanyama waweze kukua kwa haraka na ambao watakuwa na nyama nyingi yenye ubora.




Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akikagua moja ya jalada la ardhi kwenye Ofisi ya Msajili wa Hati na Nyaraka mkoani Mara mwishoni mwa wiki. Wapili kushoto ni Kamishna wa Ardhi Msaidizi mkoani Mara, Happiness Mtutwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mabula ahimiza uwajibikaji sekta ya ardhi

**Na Munir Shemweta,** MUSOMA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka watendaji wa sekta ya ardhi katika halmashauri na manispaa za mkoa wa Mara kuwajibika kwa kufanya kazi kwa bidii.

Pia amewataka kuhakikisha wanatoa hati kwa wamiliki wa ardhi pamoja na kuhamasisha ukusanyaji kodi ya pango la ardhi.

Akizungumza na watumishi wa sekta ya ardhi mwishoni mwa wiki, Dk. Mabula alisema ufanyaji kazi kwa kujituma kwa watumishi wa sekta hiyo itaiwezesha Wizara ya Ardhi kuongeza kasi ya utoaji hati na wakati huo kukusanya mapato yatokanayo na kodi ya ardhi.

Kwa mujibu wa Mabula, kwa sasa katika mkoa wa Mara kasi ya utoaji hati za ardhi pamoja na makusanyo yatokanayo na kodi ya ardhi hairidhishi na juhudi kubwa zinahitajika katika kutoa hati na kuhamasisha wamiliki kulipa kodi ili serikali iweze kupata fedha za kuendesha shughuli zake.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Mara, Hapiness Mtutwa, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 ulikusanya shilingi bilioni 1.065 sawa na asilimia 23 katika malengo ya bilioni 4, huku mwaka wa fedha 2020/2021 ukikusanya bilioni 1.7 sawa na asilimia 47.5 kati ya malengo bilioni 3.7.

"Maelekezo yangu mkafanye kazi kwa bidii katika wilaya zenu na nikikuta mtendaji wa sekta ya ardhi hafanyi haya ninayoelekeza basi ujue wewe hutufai," alisema Dk. Mabula.

Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Maendeleo ya Makazi Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Imaculata Senje, aliwataka watendaji wa sekta ya ardhi hasa wa Mipango Miji kuwa wabunifu kwa kuwaelimisha wananchi umuhimu wa maeneo yao kupimwa.

Naye Ofisa Kodi kutoka Wizara ya Ardhi, Rehema Kilonzo, aliwaeleza watendaji wa sekta ya ardhi katika mkoa wa Mara kuhakikisha wanayajua na kufuatilia kwa karibu madeni ya wadaiwa wote sugu wa kodi ya pango la ardhi.

# DCB kuboresha huduma kidigitali

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Biashara ya DCB imesema itaendelea kuboresha na kuingiza sokoni bidhaa na huduma mbalimbali za kidigitali kwa lengo la kusogeza huduma zake karibu kwa wateja, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha Watanzania wanazipata kwa haraka na gharama nafuu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Biashara wa DCB, Zacharia Kapama, alisema uboreshaji wa huduma zao kibenki kwa njia ya kidigitali unaonyesha nia ya kufanya benki hiyo kuzidi kupiga hatua na kuwa chaguo namba moja kwa kila anayehitaji huduma za kifedha nchini kwa haraka na gharama nafuu.

"Uboreshaji wa huduma za kibenki kidigitali ni moja ya mikakati ya DCB katika kuhakikisha benki yetu inakwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na kiteknolojia yanayoendelea duniani kote katika kubuni mbinu rahisi na za haraka za kufikisha huduma za kibenki karibu na mteja," alisema Kapama.

Alisema DCB kwa kitambo sasa imeendelea kutoa huduma mbalimbali kwa njia ya mtandao, mwaka 2018 ilizindua huduma za DCB Pesa na kusajili wateja zaidi ya 200,000 wanaotumia huduma zao za kidigitali. Huduma hizi zilipokelewa kwa mwamko mkubwa na hadi leo wateja wa DCB wanaweza kukopa na kufanya marejesho kwa njia ya kidigitali.

Alisema kutokana na mabadiliko ya chapa ya benki yao waliyokamilisha miezi michache iliyopita, sasa imeendelea kuja na njia mbalimbali za kutoa huduma kidigitali huku wakitambua kuwa dunia ya sasa imekuwa ya kidigitali huku kila tasnia ikiongeza ubunifu katika kubuni teknolojia zikazofanya suala la utoaji huduma mbalimbali lifanyike kwa haraka, rahisi na ubora.

Vile vile, alisema sasa wananchi wote wanaweza kulipa kodi na ushuru kupitia mfumo mpya wa malipo ya serikali (GePg) katika matawi yote ya benki hiyo na kupitia huduma za kimtandao na kwa njia ya simu.

Kuhusu mfumo wa mawakala wa DCB, Mkurugenzi huyo alisema benki imeboresha mtandao imara wa mawakala kwa kuanzisha mawakala wakubwa (Super Wakala) unaohudumia wateja bila uhitaji wa kufika katika matawi nchi nzima. Vilevile benki imesogeza huduma za kibenki kwenye manispaa zote za Dar es Salaam na mikoani lengo likiwa ni kuwarahisishia wananchi kufanya miamala kwa haraka na nafuu.

# Shule zaagizwa kuwapa chakula wanafunzi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amewataka viongozi wa halmashauri zote na watendaji wa afya kitengo cha lishe kuhakikisha chakula kinapatikana kwenye shule zote.

Kunenge alitoa maelekezo hayo mwishoni mwa wiki katika kikao kazi cha tathmini ya mkataba wa lishe katika Mkoa wa Pwani kilichofanyika mjini Kibaha.

Alisema lishe bora katika jamii ni kichocheo cha maendeleo endelevu katika nyanja zote hususani ya viwanda, afya, kilimo, elimu, biashara na uchumi, lakini hayo yatafikiwa endapo athari za lishe duni zitadhibitiwa.

Alisema hali ya udumavu kwa mkoa huo ni asilimia 23.8 ukilinganisha na ya Taifa asilimia 30.1 (TNNS, 2018).

"Tafsiri yake ni kuwa katika watoto 100 wenye umri chini ya miaka mitano, watoto 24 wamedumaa na hata wakiwa watu wazima itakuwa ngumu kwao kuinua uchumi wa familia na taifa kwa ujumla," alisema Kunenge.

Kunenge aliongeza kuwa katika kila darasa lenye watoto 45, watoto 11, wanaweza kuwa wadumavu na hawafundishiki, hivyo ni vyema kusisitiza upatikanaji wa chakula shuleni.

"Upatikanaji huu unaweza kufanyika kwa shule kuzalisha matunda, mboga na mazao ya chakula kama vile mihogo, mahindi na mpunga pia ufugaji wa wanyama wadogo wadogo kama kuku, bata na sungura kulingana na hali halisi ya maeneo ya shule," alisisitiza. Amesema endapo utekelezaji huo utafanyika ni dhahiri kwamba watoto shuleni watakuwa na afya bora na wataweza kuelewa wanayofundishwa.

Alizipongeza halmashauri zote tisa za Mkoa wa Pwani kwa utekelezaji mzuri wa mkataba wa lishe kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2021.

Ofisa lishe Mkoa wa Pwani, Pamela Meena, alisema kwa sasa wanakabiliwa na kikwazo cha uhaba wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii waliojengewa uwezo katika masuala ya lishe na usimamizi usioridhisha wa mkataba wa lishe ngazi ya kata, vijiji na mitaa.



Mdhibiti wa Mafunzo wa TBL, Albertho Mramba (kushoto), akitoa maelezo ya shughuli za kampuni kwa wafanyakazi wa vyombo vya habari vya EFM na ETV walipofanya ziara katika kiwanda cha bia cha Ilala, mkoani Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TASAF yajenga wodi ya mama, mtoto

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) imetoa Sh. milioni 193 kwa ajili ya kujenga wodi ya mama na mtoto kwenye Zahanati ya Kijiji cha Mkambarani, wilayani Morogoro, ili kuboresha huduma ya afya ya uzazi.

Fedha hizo zimetolewa ikiwa ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa ya Machi 14, mwaka huu ya kukagua utekelezaji wa miradi ya TASAF mkoani Morogoro.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Mkambarani, Ndejembi, alisema wakati wa ziara ya Kamati ya Bunge, wananchi walieleza kikwazo cha upatikanaji wa huduma ya afya ya uzazi kinachowakabili kinamama wanapohitaji huduma hiyo.

Alisema kamati hiyo iliishauri serikali kuangalia uwezekano wa kutatua kikwazo hicho ili kuwaondolea adha kinamama wa Kijiji cha Mkambarani kusafiri umbali mrefu kufuata huduma hiyo katika Kituo cha Afya Kingolwira ama Morogoro Mjini.

Naibu waziri huyo aliwaasa watendaji wa serikali wenye jukumu la kusimamia ujenzi huo kwenye Zahanati ya Mkambarani kuhakikisha fedha iliyotolewa inatumika kujenga wodi ya mama na mtoto kama ilivyokusudiwa.

Ndejembi alisema, serikali imetoa fedha hizo kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa wodi ya mama na mtoto ili wananchi wa Mkambarani wapate huduma bora.

Naibu Waziri alisema, fedha hizo zimeingizwa katika akaunti ya Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro kwa ajili ya kujenga wodi hiyo na kuagiza ujenzi ujengwe kwa kutumia Force Account.

Aliwataka walengwa wa TASAF ambao ni kaya maskini ambazo hupewa ruzuku na mfuko huo kutumia vizuri ruzuku wanayoipata kujikwamua katika lindi la umaskini ili baadaye waache kutegemea fedha hizo.

Naye Mratibu wa TASAF Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Eustaki Moshi, akitoa taarifa ya mafanikio ya TASAF III kwa Naibu Waziri alisema, walengwa kwa kupitia ruzuku wameweza kupata fedha ambayo inawasaidia kulima mashamba, kuanzisha biashara ndogo na ufugaji wa mifugo.

# 249 wadahiliwa shule zilizojengwa na GGML

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya wanafunzi 249 wamedahiliwa kuanza masomo ya kidato cha tano kwa mwaka wa masomo wa 2021/2022 katika shule za Bugando na Kamena mkoani Geita ikiwa ni mwendelezo wa mipango ya Kampuni ya Geita Gold Mine Ltd. - GGML kuboresha mazingira ya elimu mkoani humo.

Shule hizo ambazo ni za serikali zilijengwa na kampuni hiyo kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Geita kwa gharama ya Sh. milioni 287.5 kupitia mfuko wa uwajibika kwa jamii wa kampuni hiyo.

Kaimu Ofisa Elimu, Taaluma kwa Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Navaya Alphonce, alisema tangazo la kuanza kupokea wanafunzi hao kwa shule hizo limepokewa kwa furaha na wananchi wa mkoa wa Geita na wadau wote ikiwamo GGML." "Udahili wa wanafunzi ni mafanikio makubwa kwa sekta ya elimu nchini na sasa wanafunzi wameanza kuhudhuria masomo vyema.

"Tunaamini kwamba Kamena na Bugando ni mifano ya jinsi shule nzuri inapaswa kuwa kwa sababu shule zote zina mazingira yanayomfaa mwanafunzi kusoma na tuna imani tutashika nafasi ya juu na kushindana kimasomo na shule zingine zinazoongoza nchini," alisema.

"Ingawa tuna mihula miwili katika mwaka wa masomo, kati ya wanafunzi 249 katika shule zote mbili hatujapokea taarifa kutoka kwa mzazi yeyote anayeomba kumhamisha mtoto wake kutoka katika shule hizi. Hii ni uthibitisho kwa walimu na wafanyakazi wote wa shule hizi kujitolea wa kufundisha kwa bidii ili kusaidia wanafunzi hawa wa Kamena na Bugando kufanya vizuri," alisema

Alisema shule hizo zilijengwa kwa bajeti ya pamoja ya Sh. milioni 287.5 na kuungwa mkono na GGML na Halmashauri ya Wilaya ya Geita chini ya mpango wa Uwajibikaji wa Jamii kwa Jamii wa 2018.

# Mwambe agawa pikipiki jimboni

**Na Paul Mahundi,** MTWARA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) ambaye ni Mbunge wa Masasi, Geoffrey Mwambe, amekabidhi pikipiki 25 kwa kikundi cha bodaboda kilichoko wilayani hapa.

Waziri Mwambe alizigawa pikipiki hizo akiwa kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika viwanja vya Uwanja wa Fisi, Masasi mjini na kuwasisitiza bodaboda hao kuwa mpango huo utakuwa endelevu kwa kuwa wahitaji wa pikipiki hizo wamekuwa wengi, na kuahidi kufanikisha upatikanaji wa zingine kwa siku za usoni. "Natambua maombi ya walioomba pikipiki yalifika 200, lakini tulipitia tukaona wanaokidhi vigezo ni 25, hivyo niwaahidi mchakato huu hautoishia hapa bali utakuwa endelevu kwa awamu nyingine," alisema Mwambe.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Claudia Kitta, alimpongeza mbunge huyo kwa jitihada zake za kufanikisha upatikanaji wa bodaboda hizo ambazo zimefungua ajira kwa vijana ishirini na tano kwa wakazi hao.

Naye Mwenyekiti wa bodaboda hao, Selemani Mohamed Ajali, alimshukuru mbunge huyo kwa kufanikisha mikopo ya pikipiki hizo ambao una masharti nafuu kwao kuweza kuyamudu.

# Shule zapigwa jeki viti, mabati

Na Beatrice Moses

SHULE kadhaa Wilaya ya Ubungo mkoani Dar es Salaam zimepatiwa msaada wa viti, meza na mabati msaada huo umetolewa na Benki ya NMB, kupitia programu ya Uwajibikaji kwa Jamii ambao ni viti na meza 150 kwa shule za sekondari Saranga ya Kimara na Mashujaa ya Sinza, pamoja na mabati 175 kwa Shule ya Msingi Mianzini, iliyopo Magomeni Makurumla, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 20.

Hafla ya makabidhiano hayo ilifanyika katika Shule ya Sekondari Saranga, ambako Mkuu wa Kitengo cha Biashara za Serikali wa NMB, Vicky Bishubo, alimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Heri James, mbele ya Mbunge wa Ubungo na Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo.

Bishubo alisema msaada huo ni sehemu ya utaratibu wao wa kila mwaka, ambako hutumia asilimia moja ya faida yao kwa mwaka uliotangulia, kurejesha kwa jamii kwa kusaidia utatuzi wa changamoto zinazoikabili Sekta za Elimu na Afya, pamoja na majanga.

Bishubo alibainisha kuwa, NMB inatambua, kuthamini na kuunga mkono jitihada za Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan katika kuboresha mazingira ya vijana na watoto wa Kitanzania kupata elimu bora, hivyo wao kama wadau, wanao wajibu wa kusapoti jitihada hizo kwa kusaidia kila penye uhitaji.

"Benki yetu inatambua namna serikali inavyopambana kuhakikisha inasukuma mbele sekta ya elimu na afya nchini, nasi NMB kila mwaka tunatenga asilimia 1 ya faida yetu ili kuunga mkono jitihada hizo, ambako kwa mwaka huu benki imetenga Sh. bilioni 2.

"Hadi sasa NMB imetumia Sh. bilioni 1.3 kutoa misaada kuanzia Januari hadi Agosti mwaka huu, ambapo kwa mkoa wa Dar es Salaam peke yake, benki imetoa misaada yenye thamani ya Sh. milioni 207.9, kati ya hizo Sh. milioni 144.5 katika elimu na Sh. milioni 93 sekta ya afya," alisema Bishubo.

DC James, aliishukuru NMB, aliyoitaja kama sehemu ya familia ya maendeleo wilayani mwake kutokana na ushiriki wao wa mara kwa mara wa utatuzi wa changamoto katika elimu na afya, huku akiwataka walimu na wanafunzi kutunza misaada hiyo, ili idumu kwa muda mrefu.

Naye Prof. Mkumbo aliishukuru NMB kwa namna inavyomsaidia kutekeleza ilani ya chama iliyomwingiza madarakani na kwamba heshima ya wabunge wengi nchini imejengwa na kuendelea kujengwa na benki hiyo, kadri inavyojitoa kufanya utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazoikumba jamii.




Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Prof. Zacharia Mganilwa (kulia), akibadilishana mikataba na Mkurugenzi wa Mipango wa MS-TCDC, Sara Ezra Teri, baada ya kuitia saini mikataba hiyo, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NIT yapewa siri uzalishaji wataalamu wabobezi anga

Na Prosper Makene

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimeshauriwa kuendelea kuingia makubaliano na wadau wa sekta ya usafirishaji wa ndani na nje ya nchi ili kupata msaada mkubwa wa kuzalisha wataalamu wa kutosha na wabobezi ambao watakidhi mahitaji ya soko.

Akizungumza kabla ya kushuhudia mikataba miwili iliyoingiwa kati ya NIT na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) pamoja na Kituo cha Mafunzo na Uhusiano wa Kimataifa (MS TCDC) katika kuboresha usawa wa jinsia, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Hamza Johari, alisema ni muhimu sana kuendelea kuingia katika makubaliano na wadau wa sekta ya usafirishaji ili tuweze kuzalisha wafanyakazi wa kutosha na walioiva, ambao watakidhi mahitaji ya sekta ya usafirishaji.

Johari, ambaye alikuwa mgeni rasmi aliongeza: "Mikataba hii ambayo NIT inasaini na LHRC na MS-TCDC itaweza kuboresha kwa kiasi kikubwa eneo la jinsia na usawa katika mafunzo yanayotolewa chini ya Mradi wa EASTRIP ambao unatekelezwa na NIT."

Mkurugenzi Mkuu wa TCAA ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya NIT kwenye Kituo cha Umahiri cha Taaluma za Usafiri wa Anga na Operesheni za Usafirishaji alisema ana uhakika kwamba baada ya kusainiwa kwa makubaliano haya, mradi wa Benki ya Dunia uliotekelezwa na chuo utaboreshwa sana hasa katika eneo la jinsia.

Johari ambaye ni Mwenyekiti wa Shirika la Huduma za Usafiri wa Anga (CANSO) kwa Afrika, aliongeza:

"Tunataka kuona NIT kinakuwa mahiri sana kwenye sekta ya usafirishaji, wiki iliyopita nilipokuwa kwenye mkutano mkuu wa CANSO ambapo mimi ni mwenyekiti wa Afrika, maazimio yalikuwa ni kuwa na vituo vya umahiri katika sekta ya usafiri wa anga. Kwa bahati nzuri kwenye nchi yetu tayari tunacho NIT."

Kwa upande wake Mkuu wa Chuo cha NIT Mhandisi, Prof. Zacharia Mganilwa alisema: "Tumeamua kuingia makubaliano na LHRC pamoja na MS TCDC ili waweze kutusaidia katika eneo la jinsia kwenye mradi tunaoutekeleza wa EASTRIP unaodhaminiwa na Benki ya Dunia."

Prof. Mganilwa aliongezea kuwa mashirika hayo mawili ya LHRC na MS-TCDC ni wabobezi katika eneo la jinsia, hivyo kwa kiasi kikubwa wataweza kuisaidia NIT kufikia malengo yaliyowekwa na mradi huo.

Prof. Mganilwa alisema mara nyingi masomo ya uhandisi yamekuwa yakitawaliwa sana na jinsia ya kiume na kuiacha nyuma jinsia ya kike, hivyo kwa ushawishi wa mashirika hayo mawili, chuo kinategemea mabadiliko makubwa katika kuleta usawa wa kijinsia katika eneo hilo.

"Tunatumahi kuwa taasisi hizi mbili zitatoa ushawishi mkubwa zaidi kwa wanafunzi wa kike kuchagua programu hizo ambazo zilikuwa zinasomwa na wanaume wengi zaidi ya wanawake," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alisema: "Tunaahidi kutekeleza majukumu yetu ambayo tumekubaliana ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo kwenye masuala ya jinsia wanafunzi pamoja na walimu kama inavyotakiwa na mradi wa EASTRIP."

Naye Mkurugenzi wa Mipango wa MS-TCDC, Sara Ezra Teri, alisema: "Shirika letu linatoa programu za masomo ambazo zinalenga kuimarisha uongozi bora, utawala katika maeneo ya maendeleo katika nchi za Afrika. Hivyo, kwa makubaliano haya, tunaahidi kutoa maarifa bora kwenye eneo la jinsia kwenye uendelezaji wa mitaala ili kuweza kuweza kuboresha usawa wa kijinsia. "

# Prof. Mkumbo: Vijana msikate tamaa ya maisha

Na Sabato Kasika

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, amewataka vijana kutokata tamaa katika kutafuta maisha, wajishughulishe zaidi, huku serikali ikiendelea kuwaka mazingira mazuri ya biashara, uwekezaji na ubunifu.

Prof. Mkumbo alisema hayo juzi kwenye hafla ya kukabidhi hundi yenye thamani ya Sh. milioni 550 kwa vijana 55 waliofanikiwa kupata matangazo kupitia mchakato uitwao 'Mchongo wa Big Joe'.

Vijana hao walichujwa kutokana na michanganuo yao ya biashara ambapo 55 kati yao michanganuo yao ilifanikiwa kupata mchongo wa ajili ya biashara na kila mmoja kukabidhiwa Sh. milioni 10.

"Lengo la serikali ni kuweka mazingira mazuri ya biashara, uwekezaji na ubunifu nchini, hivyo serikali inawaahidi kuwapa ushirikiano wa kutosha vijana na hata wadau wanaowawezesha," Prof. Mkumbo alisema.

Alisema, yeye ni miongoni mwa watu waliofaidika kupitia binafsi hasa vituo vya redio, kwa kuzungumza mambo mbalimbali, na kwamba serikali inathamini mchango wa taasisi hizo katika kuongeza ajira kwa vijana.

"Natoa pongezi kwa niaba ya serikali, kwa uongozi wa Clouds Media Group (CMG) kupitia Mkurugenzi Mtendaji Joseph Kusaga (Big Joe) kwa mchango wake mkubwa wa kuisaidia serikali kutoa ajira kwa vijana nchini," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, alisema, serikali inatambua mchango wa sekta binafsi katika kutoa ajira, na kwamba itaendelea kushirikiana nayo kadri inavyowezekana.

Akizungumza kwa niaba yake, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, alisema, serikali inaweka mazingira mazuri, ili kuhakikisha vijana wanajiajiri kwa shughuli mbalimbali.

"Tunaunga juhudi zote zinazofanywa na Watanzania kwa lengo la kuwasaidia vijana kujiendeleza au kujiajiri, hivyo ninaahidi kuendelea kufanya kazi nao bega kwa bega," alisema Makalla.

Naye Mkurugenzi wa CMG, Joseph Kusaga, aliwataka vijana waliopata bahati ya kupen-

Nipashe
Spotika



USAJILI 10 GHALI TANGU MLIPUKO WA COVID-19L UK. 12-13



# SABABU 4 KWA NINI MESSI AJIUNGE NA PSG

**PARIS, Ufaransa**

LIONEL Messi na Barcelona wanaachana, huku PSG ikitajwa kuwa ndio yenye nafasi ya kuinasa saini yake. Tumesikia hapo awali, lakini wakati huu inasikika kama ya kweli. Baada ya kushindwa kupokea msaada kutoka kwa LaLiga katika harakati zao za kumpa mkataba mpya Messi, inaonekana wazi kwamba Barcelona wamenyanyua mikono juu.

Tangazo hilo lilitolewa Alhamisi usiku, wakati Barcelona ilisema makubaliano na Messi hayatatekelezeka kwa sababu ya kanuni za kifedha zilizowekwa na LaLiga. Tangu habari hiyo itokee, ulimwengu umekuwa na hamu ya kujua ni wapi Messi atakakoelekea.

Hakuna ubishi kwamba PSG wamekuwa wakimpenda Messi kwa muda mrefu. Mara tu baada ya Barcelona kuthibitisha kutokuwa na uwezo wa kubaki na huduma ya mshambuliaji huyo, PSG haikupoteza muda kuwasiliana na Messi.

Inaeleweka, PSG wanaamini kabisa kwamba, kumshawishi Messi kwenda Paris kunaweza kumaliza kusubiri kwao kuinua taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Nyongeza hiyo kwa misuli yao ya kifedha na utafikiria ushirika kati ya PSG na Messi ni suala la lini.

Huku mazungumzo yakitarajiwa kukusanya kasi katika siku zijazo, hapa kuna sababu nne kwa nini Messi anapaswa kuifanya PSG kuwa ndio kituo chake cha pili kinachofuata, sasa zifahamu...

**#4. Messi atahisi yuko nyumbani**

Hakuna kitu kinachohisi kama nyumbani, lakini maeneo fulani au watu huja karibu nayo. Mbali na kocha mkuu Mauricio Pochettino, kuna wachezaji wengine watatu wa kikosi cha kwanza kutoka Argentina kule PSG. Wapo Angel Di Maria na Leandro Paredes.

Kwa sababu ya uwapo wa msingi thabiti wa Argentina, Messi anaweza kutulia kwenye mazingira mapya na kuzingatia mpira wake mara moja. Baada ya kushinda Copa America mwezi uliopita kwa Argentina pamoja na Di Maria na Paredes, tayari kuna uelewa na umoja kati yao.

Ingawa Messi hajawahi kushirikiana na Muargentina mwingine, Mauro Icardi kwa sababu za kibinafsi, sababu hiyo haitarajiwi kufifisha uamuzi wake wakati wa kujiunga na mradi huo pale PSG. Inaweza kuwa maelezo tu na PSG inaweza hata kuwa tayari kuachana na Icardi na kumsajili Messi.

**#3. Kumaliza ukame Ligi ya Mabingwa Ulaya**

Wote PSG na Messi wamekuwa na wakati mbaya wa kudhalilika katika michuano ya Ligi ya Mabingwa katika misimu ya hivi karibuni. Kwa hivyo, njaa na hamu ya kupata taji la michuano hiyo itakuwa kubwa zaidi kwa pande zote mbili.

Katika jaribio lao la kujaribu kwenda mbali kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, PSG imesajili wachezaji bora katika msimu huu wa joto. Washindi wa zamani wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Sergio Ramos na Georginio Wijnaldum walijiunga na PSG kwa uhamisho wa bure, wakati pia klabu hiyo ilishangilia usajili wa Achraf Hakimi kutoka Inter Milan.

Kwa kuongezea, kusajiliwa kwa Gianluigi Donnarumma kwenye uhamisho mwingine wa bure kumesaidia PSG kukusanya mkusanyiko wa wachezaji wengi nyota kwa msimu ujao.

Ikiwa Messi ataamua kuhamia Paris katika siku zijazo, itazingatiwa kama kipande cha mwisho kwenye fumbo. Ni aina ya saini ambayo inaweza kumaliza kusubiri kwao kwa muda mrefu kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Baada ya kushiriki mara kwa mara katika hatua za mwisho za Ligi ya Mabingwa Ulaya katika misimu miwili iliyopita, na kwa kuzingatia jinsi walivyoimarisha safu yao, PSG inashika nafasi ya kwanza kwenye orodha ya maeneo ambayo Messi anaweza kung'ara.

**#2. Muunganiko na Neymar**

Sio siri kwamba, Messi na Neymar wangependa kuungana tena pale PSG. Mbali na kuheshimu uwezo wa kila mmoja, wawili hao pia walifurahia mpira wao mzuri wakati wakicheza pamoja kule Barcelona.

Kufuatia habari za Barcelona kufungwa mikono na kanuni za LaLiga, mazungumzo ya kuungana tena kwa wawili hao kule PSG yamekuwa yakiendelea.

Neymar ameripotiwa hata kuwa tayari kutoa jezi yake namba 10 kwa Messi.

Hakuna ubishi kwamba, wawili hao wanaweza kuwasha moto wa hatari pale PSG. Ikiwa makubaliano hayo yatapita, Messi atafurahia fursa hiyo ya kuongeza urafiki wake uwanjani na Neymar.

Ripoti za hivi karibuni zimedokeza kwamba Neymar amekuwa akiweka shinikizo kwa PSG kujaribu kupata mkataba kwa Messi mapema zaidi.

**#1. Kumaliza ubishi wa nani bora**


Messi anatajwa ana nafasi kubwa ya kushinda tuzo ya saba ya Ballon d'Or mwaka huu. Lakini hata hivyo, sehemu zingine za ulimwengu wa soka zinaamini Muargentina huyo anahitaji kujiimarisha sehemu nyingine nje ya Hispania ili kuwa bora zaidi.

Cristiano Ronaldo amefanikiwa katika hilo, hivyo ni kawaida watu kutegemea pia Messi atafanya hivyo. Kama akijiunga na PSG, ni wazi kwamba Messi anaweza kumaliza ubishi wa nani zaidi kwenye ubora.

Baada ya kufunga mabao 672 na kushinda mataji 34 tangu alipoanza kuichezea Barcelona mwaka 2004, ni wakati sasa kwa Messi kutafuta changamoto nyingine.

## ISIKUPITE

LIONEL Messi ambaye anaachana na Barcelona, ndiye mchezaji pekee aliyefunga mabao mengi (672) katika klabu moja katika historia ya soka duniani, akifuatiwa na Cristiano Ronaldo (Real Madrid) mabao 450 na Robert Lewandowski (Bayern Munich) mabao 294.



# USAJILI 10 GHALI TANGU MLIPUKO WA COVID-19


SANCHO

**LONDON, England**

MLIPUKO wa ugonjwa wa COVID-19 mwaka jana ulilazimisha ligi kubwa zote duniani kusimama, huku msimu ukimalizika miezi kadhaa mbele na viwanjani pia kukiwa hakuna mashabiki.

Kukosekana kwa mashabiki viwanjani kulisababisha hasara kubwa ya kupoteza mapato kwa klabu, huku pia kukisababisha soka la usajili wa wachezaji kuwa gumu.

Mlipuko wa ugonjwa huo umeziyumbisha klabu nyingi kiuchumi, mikopo ndio imekuwa suluhisho kwa timu kuweza kujinusuru.

Matokeo yake, usajili wa fedha kubwa ukawa ni mdogo kwani klabu zimeteteteka sana kiuchumi.

Kutokana na hilo, makala haya inaangalia usajili 10 ghali zaidi kufanywa tangu mlipuko wa COVID-19 mwaka jana, twende sasa...

**#10. Ben Chilwell (Chelsea) - Euro milioni 50.2**

Mshindi wa Kombe la Ligi Kuu ya England na Leicester City, mlinzi Ben Chilwell alinaswa na Chelsea kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Mlinzi huyo wa kushoto alicheza mechi 40 kwenye mashindano yote msimu uliopita wakati 'Blues' hao wakifanya mabadiliko ya makocha.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, alikuwa sehemu ya nguzo muhimu kwa Chelsea akitoa pasi tano za mabao na kufunga matatu wakati wakishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Alicheza kwa mara ya kwanza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kipindi cha miaka minne, na Chilwell alifunga bao moja katika mechi kumi wakati Chelsea ikishinda taji hilo kwa mara ya pili katika historia yake. Hata hivyo, Chilwell hakuitwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya England kwenye michuano ya Euro 2020, kwani Luke Shaw ndio alikuwa chaguo namba moja kwa nafasi ya beki wa kushoto.

**#9. Timo Werner (Chelsea) - Euro milioni 53**

Chelsea ilizishinda Liverpool na Manchester City katika mbio za kuwania saini ya Timo Werner kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Baada ya kuanza vizuri pale katika dimba la Stamford Bridge, Werner akajikuta akikabiliwa na wakati mgumu wa kuwa na ukame wa kufunga kwa muda mrefu. Lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, alifanikiwa kurudisha namba yake katika kikosi cha kanza.

**#8. Ben White (Arsenal) - Euro milioni 58.5**

Ben White alikuwa sehemu muhimu kwa kikosi cha Leeds United kilichomaliza nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, baada ya kurudi katika ligi hiyo kwa kipindi cha muongo mmoja.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, mlinzi wa kati alicheza mechi zote za ligi kasoro mbili na alikuwa kwenye kiwango cha kuvutia sana na akavutia hisia za Arsenal na wamemsajili.

Ujio wa White pale Arsenal unakwenda kuimarisha safu ya ulinzi ya kikosi hicho ambacho msimu uliopita kilishindwa kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya au Ligi ya Europa msimu unaoanza.

**#7. Miralem Pjanic (Barcelona) - Euro milioni 60**

Miralem Pjanic aliwasili Barcelona kipindi cha majira ya joto kilichopita katika dili ambalo lilimhusisha Arthur Melo kwenda Juventus.

Hata hivyo, Pjanic hakuwa na mchango mkubwa pale Camp Nou tofauti na matarajio. Kiungo huyo wa Bosnian alishindwa kufunga wala kutoa pasi ya bao katika mechi za mashindano yote na alikuwa na wakati mgumu kupata nafasi ya kucheza kikosi cha kwanza cha Barcelona.

Mwaka mmoja baada ya kuwa mgumu kwake kule Barcelona, kiungo huyo ameripotiwa kurudi Juventus.

**#6. Achraf Hakimi (PSG) - Euro milioni 60**

Achraf Hakimi ni mmoja wa walinzi wa pembeni vijana ambaye ni mfungaji mzuri kwa sasa.

Baada ya kucheza kwa mafanikio kwa mkopo kule Borussia Dortmund, klabu yake ya Real Madrid ikamuuza raia huyo wa Morocco kwenda Inter Milan msimu uliopita. Hakimi alikuwa kwenye kiwango bora, akifunga mabao saba na kutoa pasi za mwisho 10 na pia kuwasaidia Inter kushinda taji lao la kwanza la Scudetto kwa kipindi cha muongo mmoja.

Hata hivyo, wakati PSG walipomtaka kwa ofa ya euro milioi 60, nyota huyo mwenye umri wa miaka 22, akaondoka Inter Milan ambako amecheza kwa msimu mmoja tu. Cha kufurahisha Inter walimnunua kwa euro milioni 54 kipindi cha majira ya joto kilichopita.

**#5. Ruben Dias (Manchester City) - Euro milioni 68**

Ruben Dias alikuwa mmoja wa usajili bora kipindi cha majira ya joto msimu uliopita. Baada ya kuwasili pale Manchester City, Dias haraka akazoea maisha ya soka la Uingereza.

Akiwa kwenye kiwango cha kuvutia aliisaidia City kushinda taji lao la tatu la Ligi Kuu ya England kwa kipindi cha miaka minne na kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 24, ambaye aliwahi kuichezea Benfica, alishinda tuzo ya mchezaji bora wa Ligi Kuu wa msimu uliomalizika.

**#4. Victor Osimhen (Napoli) - Euro milioni 70**

Baada ya kufanya vizuri kule Lille, Victor Osimhen aliwasili Napoli kipindi cha majira ya joto kilichopita kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo ya euro milioni 70.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, alikuwa mmoja wa wafungaji bora vijana katika ligi kubwa tano Ulaya, akifunga mabao 10 ya ligi.

Licha ya kwamba anatajwa kuwaniwa na klabu nyingi kubwa Ulaya, Osimhen anatarajiwa kuendelea kubaki hapo Napoli.

**#3. Arthur Melo (Juventus) - Euro milioni 72**

Arthur Melo aliwasili Juventus katika dili lililomhusisha Miralem Pjanic kwenda upande wapili, Barcelona.

Mwaka mmoja baadaye, ni rahisi kusema kwamba, 'Bianconeri' hao walikuwa na dili zuri zaidi. Hiyo ni kwa sababu ingawa raia huyo wa Brazil alifunga bao moja katika mechi 31 za mashindano yote, Arthur alikuwa na kiwango bora kabisa.

Na sasa ni suala la kusubiri kuona tu kama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 ataweza kuwa kwenye kiwango bora zaidi msimu huu.

**#2. Kai Havertz (Chelsea) - Euro milioni 80**

Kai Havertz aliwasili pale Chelsea msimu uliopita na kiungo huyo mwenye umri wa miaka 22, alifunga hat-trick kwenye Kombe la Ligi, lakini alifunga mabao manne tu kwenye Ligi Kuu.

Kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, raia huyo wa Ujerumani alifunga bao ambalo liliwapa Chelsea ubingwa huo.

**#1. Jadon Sancho (Manchester United) - Euro milioni 85**

Manchester United hatimaye walifanikisha usajili wa Jadon Sancho, ambapo walitoa kiasi cha euro milioni 85 ili kukamilisha uhamisho wake kipindi hiki cha majira ya joto.

Sancho mwenye umri wa miaka 21, alikuwa na muda wa mafanikio kwa kipindi cha misimu minne aliyocheza kule Borussia Dortmund, akifunga mabao 50 na kutoa pasi za mwisho 64 katika mashindano yote.

Alikuwa mmoja wa wachezaji watatu wa England waliokosa penalti kwenye fainali ya euro 2020 dhidi ya Italia na sasa anasubiriwa kuonyesha kipaji chake pale Old Trafford.

Kadhalika, anasubiriwa kuonyesha kiwango chake kama ilivyokuwa kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

## Nukuu

"Hakuna kitakachokuwa sawa tena. Wala Camp Nou, wala Jiji la Barcelona, wala sisi wenyewe. Baada ya zaidi ya miaka 20 kwenye klabu, utaacha kuvaa jezi ya Barça. Ukweli, wakati mwingine, ni vigumu sana. Sisi tulikutana mnamo mwaka 2000, tulikuwa na umri wa miaka 13 na kazi ya mbele. Ni kazi gani! Mama ambaye alituzaa! Ikiwa tungeibuni wakati huo, isingewezekana kuifanya vizuri zaidi! " **Beki wa Barcelona, Gerard Pique akitoa hisia zake kwa Lionel Messi kuondoka katika klabu hiyo ya Camp Nou.**



"El Clasicos [Barca vs Real Madrid] ndani ya La Liga inaekelea kuwa tofauti. Hapo awali, kamera zilikuwa za Cristiano [Ronaldo] na Messi [Lionel]. Sasa watu bado wataendelea kutazama, lakini haitakuwa sawa. Soka limebadilika sana, kuondoka kwa Messi Barcelona kunathibitisha hilo, **" Nyota wa Everton, James Rodriguez akizungumzia mwonekano wa LaLiga baada ya Messi kutangazwa kuachana na Barca.**



"City ni timu bora nchini ikiwa na kocha anayechukuliwa kuwa bora zaidi duniani, [kutua Man City] ni ndoto iliyokuwa kwenye sehemu ya klabu kama hii," **Kiungo wa England, Jack Grealish baada ya City kumsajili kwa pauni milioni 100 akitokea Aston Villa.**






Mchezaji mpya wa Yanga raia wa Msumbiji kutoka klabu ya UD Songo, Jimmy Ukonde, akikokota mpira kuelekea lango la wapinzani wao, Express ya Uganda katika mechi ya Kombe la Kagame iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana na Yanga kuchezea kichapo cha mabao 3-1. **MPIGAPICHA WETU**

# YANGA HOI REKODI YA SIMBA, KAGAME

**Na Adam Fungamwango**

KIPIGO cha mabao 3-1 dhidi ya Express ya Uganda Jumamosi, kimemaliza ndoto za klabu ya Yanga kutwaa Kombe la Kagame kwa mara ya sita na kuifikia rekodi iliyowekwa na Simba.

Kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga ilishindwa kabisa kuwakabili Waganda hao waliokuwa wakiongozwa na mchezaji wa zamani wa Simba, Juuko Murshid na kufifisha ndoto hiyo.

"Tunawataka wanachama na mashabiki wa Yanga kuja kwa wingi kuisapoti timu yetu kwani tunataka kuchukua kombe hili kwa mara ya sita. Lakini haiwezekani lichezwe nchini halafu lichukuliwe na klabu nyingine kutoka nje." Yalikuwa ni maneno ya Ofisa Habari wa Klabu ya Yanga, Hassan Bumbuli, siku chache kabla ya kuanza michuano hiyo.

Simba ndiyo Mabingwa wa Kihistoria wa michuano hiyo, ikichukua mara sita.

Ilikuwa ni Yanga pekee kwenye michuano hiyo ndiyo iliyokuwa na rekodi ya kuifikia Simba, kwani timu zingine ambazo zimechukua kombe hilo mara tano kama Yanga hazikushiriki mwaka huu. Timu hizo ni AFC Leopards, Gor Mahia na Tusker, zote tatu ni za kutoka nchini Kenya.

Kutolewa kwa Yanga kwenye michuano hiyo, mbali na kuifanya Yanga kutoweza kuifikia rekodi ya Simba, lakini kunawaweka Mabingwa wa Kihistoria hao salama kuendelea kutamba kwenye soka la Afrika Mashariki na Kati kuwa ndiyo timu pekee iliyochukua mara nyingi, hadi hapo mwakani litakapofanyika tena.

Yanga imeshindwa kufuzu baada ya kumaliza ikiwa kwenye nafasi ya tatu kwenye Kundi A, ikimaliza ikiambulia pointi mbili tu.

Ilicheza mechi tatu, bila kushinda, sare mbili na kupoteza moja. Imefunga mabao mawili na kufunga manne.

Yanga ilianza mechi zake Agosti Mosi ilipocheza dhidi ya Big Bullets ya Malawi na kutoka sare ya bao 1-1, kabla ya kulazimishwa suluhu bila kufungana, dhidi ya Atlabara ya Sudan Kusini Agosti 4. Waganda ndiyo waliokuja kuipiga kumbo Agosti 7 kwa kuichakaza mabao 3-1. Kutokana na matokeo ya michuano hiyo inayoendelea, timu ya Express ya Uganda na Big Bullets ya Malawi zimesonga mbele kwenye hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo kwenye Kundi A.

Kwenye Kundi B, timu ya Azam imesonga mbele licha ya kuchapwa mabao 3-2 dhidi ya KMKM ya Zanzibar.

Kwa ushindi wa KMKM, timu hiyo nayo imesonga mbele ya michuano hiyo, nusu fainali ya kwanza ikitarajia kuchezwa Jumanne kati ya Express na KMKM, na Jumatano Azam itakumbana na Big Bullets ya Malawi, fainali ikitarajiwa kupigwa Jumamosi.

Hii hapa ni miaka ambayo timu za Simba na Yanga zimetwaa Kombe la Kagame.

**Miaka iliyotwaa Simba**

Mbali na kuwa ndiyo timu iliyochukua mara nyingi, lakini Simba pia ni timu ya kwanza kutwaa ubingwa wa michuano hiyo ilipoanzishwa mwaka 1974.

Ilifanyika nchini Tanzania ikichezwa kwa mtindo wa ligi. Mwaka 1991 iliichapa Villa mabao 3-1, na mwaka 1992 iliutetea ubingwa wake ilipoifunga Yanga kwa penalti 5-4 mjini Zanzibar, baada ya sare ya bao 1-1. Mwaka 1995, Simba ilitwaa tena kombe hilo kwa kuifunga Experss ya Uganda kwa penalti 5-3, likifanyika nchini, na ikatwaa tena 1996 kwa kuichapa APR ya Rwanda bao 1-0 nchini Tanzania pia. Mwaka 2002 ilitwaa mara ya sita mjini Zanzibar kwa kuifunga Prince Louis bao 1-0.

**Miaka iliyotwaa Yanga**

Yanga ililitwaa Kombe la Kagame mara ya kwanza mwaka 1975 mjini Zanzibar iliifunga Simba mabao 2-0 kwenye fainali, ikaja kuchukua tena mwaka 1993 nchini Uganda kwa kuifunga SC Villa mabao 2-1, na ikalibeba tena mwaka 1999 huko huko Uganda kwa kuifunga timu hiyo hiyo, safari hii kwa penalti 4-1, baada ya sare ya bao 1-1.

Mwaka 2011, Yanga ilitwaa tena ubingwa huo nchini Tanzania kwa kuifunga Simba bao 1-0 kwenye fainali, na mwaka uliofuata 2012 iliifunga Azam FC mabao 2-0 kwenye fainali iliyochezwa Uwanja wa Taifa, sasa Benjamin Mkapa.

**JE, WAJUA?**



KIUNGO wa Manchester United, Bruno Fernandes, ndiye mchezaji aliyetengeneza nafasi nyingi za mabao (20) katika Ligi Kuu England msimu wa 2020/21, akifuatiwa na Kevin De Bruyne (Manchester City) nafasi 19 na Trent Alexander-Arnold (Liverpool) nafasi 14 .



# Ushindani shuleni wahamasisha wazazi kupeleka watoto

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, amesema ushindani unaonyeshwa na sekta binafsi kwenye utoaji elimu umekuwa kivutio kikubwa kwa wazazi kuwapeleka watoto kwenye shule hizo.

Dk. Akwilapo alitoa kauli hiyo mwisho wa wiki wakati alipozungumza kwenye mahafali ya nane ya Shule ya Msingi El Shadai, jijini hapa.

Alisema serikali inatambua na kuuthamini mchango mkubwa elimu unaotolewa sekta binafsi hapa nchini na itaendelea kutoa ushirikiano kwa taasisi na watu binafsi waliowekeza kwenye sekta elimu.

"Lengo la ushirikiano huu ni kumsaidia mtoto kuipata elimu bora ambayo serikali ndio ingetakiwa kuwapatia haki hiyo watoto wote," alisema.

Dk. Akwilapo alisema wanafunzi wa darasa la saba watakaohitimu mwaka huu watakuwa wa kwanza kufanya mitihani yao tangu kuanzishwa kwa mtaala mpya wa masomo ulioanza mwaka 2015.

Aliutaja mtaala huo kuwa ni Kusoma Kuandika na Kuhesabu (KKK) na wanafunzi hao watapimwa kupitia mitihani ya kitaifa inayotarajiwa kufanyika Septemba, mwaka huu.

Mkurungenzi wa shule hiyo, Juliana Kalinga, aliomba serikali kupitia wizara hiyo kuangalia namba ya kuwasaidia kupata mikopo ya muda mrefu yenye riba ndogo ili kusaidia uendeshaji wa shule. Kalinga alisema hadi sasa shule ina wanafunzi 762 na wameongezeka kutokana na wazazi kuvutiwa na ufaulu mzuri wa wanafunzi wanaosoma hapo kila mwaka.

Alitaja malengo yao ni kuendeleza ujenzi wa shule ya sekondari ambayo itakuwa inawasaidia wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi kuendelea na elimu ya sekondari.

Kwa upande wake, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, John Matekele, aliomba serikali kuanzisha mitaala ya masomo ya elimu ya kujitegemea kama kilimo, lishe na ufundi ambayo yatakuwa yakiwajengea kuwa na uwezo wa kujitegemea.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo (katikati), akikagua maeneo katika Shule ya Msingi ya El Shadai iliyoko Ihumwa jijini Dodoma, alipofika kwenye mahafali ya nane ya darasa la saba ya shule hiyo mwisho wa wiki, kulia ni Mkurungenzi wa Shule ya El Shadai, Juliana Kalinga. **PICHA: IBRAHIM JOSPEH**

# Washauriwa kutoa elimu chanjo ya Uviko-19

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

WATAALAMU wa afya wameshauriwa kutoa elimu ya chanjo ya Uviko-19 kwenye maeneo ya vijijini na shuleni ili kujikinga na maambukizo ya corona.

Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustaph Rajabu, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu umuhimu wa chanjo hiyo.

Alisema kuna umuhimu wa kupeleka elimu ya kuhamasisha kupata chanjo hiyo kwa wananchi na wanafunzi vijijini kutokana na wengi wanakabiliwa na imani potofu.

Rajabu alisema kuna ulazima wataalamu hao wa afya kwa kushirikiana na viongozi wa serikali kupeleka elimu ili kuwahamasisha wajitokeze kwa wingi kupata chanjo na kujilinda na corona.

"Tunaona kwenye mitandao ya kijamii ikirushwa taarifa zinazopotosha juu ya hii chanjo baadhi ya watu wanaoishi vijijini wakiwamo na wanafunzi shuleni wamekuwa na hofu kubwa, kwa imani kuwa chanjo hiyo ina madhara, hivyo ni wakati sasa wataalamu na viongozi wa serikali na wakiwamo wa dini kushirikiana kwa pamoja ili kuiwezesha elimu hiyo kuwafikishia huko vijijini na maeneo mengineyo," alisema.

Alisema kuwa kinachoendelea vijijini ni ukosefu wa elimu ambayo itasaidia kuondokana na imani waliyonayo.

Aliwaomba viongozi wa madhehebu mbalimbali ya dini kuendelea kushirikiana na serikali katika kuwaelimisha waumini wao juu ya chanjo hiyo inayotolewa ili kuondoa imani potofu iliyojengeka kwa baadhi ya watu wanaopotosha na kutishia kuwa ina madhara.

Alisema viongozi wa dini wana nafasi kubwa ya suala hilo kwa kuwa bila jitihada zao kuna kuhakikisha wanashirikiana na serikali kuhamasisha uwezekano mkubwa suala hilo likawa zito.

Shekhe huyo aliwaomba waumini kutoka madhehebu mbalimbali ya dini kuchukua tahadhari na viongozi ambao wanaopotosha ukweli wa chanjo hiyo na wengine kuwazuia wasijitokeze kuchanja.

## Wanufaika TASAF Chamwino wajiajiri

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ASILIMIA 80 ya walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) wilayani Chamwino, wamejiajiri wenyewe baada ya kupata elimu ya kilimo cha korosho na zabibu kupitia mashamba darasa yaliyopo Kijiji cha Mlowa na Handali.

Akizungumza wakati wa ziara ya kikazi ya kutembelea miradi hiyo ya TASAF yenye lengo la kutoa ajira za muda kwa walengwa wa mpango huo, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano TASAF, Zuhura Mdungi, alisema miradi hiyo imesaidia kutoa elimu kwa walengwa na kuanzisha mashamba yao wenyewe ili kujiinua kiuchumi.

Mdungi alisema miradi ya nguvu kazi imeleta matokeo chanya kwa walengwa wa mpango huo, kwa kuwa wengi wamejikwamua kiuchumi kwa kujipatia kipato kupitia ajira za muda kwenye mashamba darasa yanayosimamiwa na viongozi wa serikali ya kijiji pamoja na waratibu wa mpango huo.

"Tunashukuru sana serikali ya kijiji, wamekuwa bega kwa bega kuhakikisha wanafanikisha kutoa elimu kwa walengwa ya kuendesha kilimo cha korosho na zabibu katika vikundi vya walengwa," alisema Mdungi.

Alisema hiyo imesaidia wengi kutoka katika kikundi na kwenda kuanzisha mashamba yao wenyewe.

Hata hivyo, aliwataka maofisa ugani kuendelea kuwapa elimu walengwa hao ili kufanikisha kilimo hicho cha muda mrefu kiwe na tija kwa wakulima.

Aliwahimiza wananchi kuendelea kuwatumia maofisa ugani ili kuwapa elimu ya kukabiliana na wadudu waharibifu wanaojitokeza shambani.

Naye, Ofisa Kilimo wa Kata ya Mlowa, Winnie Ndahani, alisema wanashirikiana na wakulima ambao ni walengwa ili kuhakikisha kilimo cha korosho kinakuwa na tija kwao.

Alisema wakulima wa Kijiji cha Mlowa wameonyesha kuvutiwa na kilimo hicho kutokana na faida kubwa na kudumu kwa muda mrefu tofauti na mazao mengine.

"Mashamba darasa yamechangia kwa kiasi kikubwa kutoa elimu kwa wakulima walengwa wa TASAF kuanzisha mashamba yao wenyewe kutokana na ujuzi walioupata," alisema.

Alitoa wito kwa wananchi wa maeneo mbalimbali mkoani Dodoma kunapokuwa na miradi hiyo ya ajira za muda inayotolewa na TASAF kufika kwa wingi ili kupata elimu.

Mlengwa wa TASAF, Yohana Malecela na msimamizi wa shamba hilo, alisema kilimo hicho ni kizuri kwa sababu ni zao la biashara tofauti na mazao mengine wanayolima. Aliishukuru TASAF kwa kuanzisha mradi huo ambao umesaidia walengwa wengi kujikwamua kiuchumi.






Magari ya mizigo yakiwa yamekwama katika Mji Mdogo wa Mbalizi juzi, baada ya malori mawili kugongana uso kwa uso kwenye mteremko wa Mlima Iwambi na kufunga barabara kwa zaidi ya saa nne. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mwalimu ajinyonga hadi kufa, mke akutwa amekufa

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MWALIMU wa Shule ya Msingi Udindilwa Kata ya Ruiwa, Wilaya ya MBARALI, Crispin Gudaga Mabena (51), amejinyonga hadi kufa kwa kutumia kamba ya katani usiku wa kuamkia juzi, Huku chanzo cha kifo chake kikidhaniwa ni wivu wa mapenzi.

Wakati huo huo, mkewe Joyce Harod (35) amekutwa amekufa chumbani kwake akihofiwa kunywa au kunyweshwa sumu.

Imeelezwa kuwa Gudaga kabla ya kifo chake alimwandikia ujumbe kaka yake kupitia simu ya mkononi pia kuacha waraka wa barua wenye kurasa mbili sebuleni ukimuhimiza kaka yake kuzingatia maagizo aliyomwachia. Hata hivyo, kaka yake hakuwa tayari kuusoma ujumbe huo kwa madai kuwa ni siri yake, hivyo atatekeleza maagizo aliyoachiwa na mdogo wake. Kwa mujibu wa mashuhuda, mkewe alimsomesha kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne na baadaye aliamua kumuoa na kumfungulia biashara. Shuhuda huyo ambaye hakuwa tayari kutaja jina lake, alisema Joyce alikuwa na mahusiano ya muda mrefu na mwanaume mwingine, na kwamba licha ya vikao vya usuluhishi mara kwa mara, hakubadilika.

Alisema kutokana na ugomvi wa mara kwa mara Gudaga aliamua kujinyonga. Akithibitisha kutokea kwa vifo hivyo, Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Mbeya, Ulrich Matei, alisema sababu ni wivu wa kimapenzi.

Hata hivyo, Kamanda Matei hakueleza kwa undani kuhusiana na matukio hayo mawili, imgawa alisema uchunguzi unaendelea.

# Mbolea mbadala Nyanda za Juu Kusini yaja

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA), imetangaza mbolea mbadala ambayo wakulima wanaweza kuipata kwa gharama nafuu.

Imeelezwa kuwa mbolea hiyo ina tija ikilinganishwa na ile iliyozoeleka aina ya Dap na Urea ambayo kwa sasa imepanda mbei na kusababisha malalamiko makubwa kutoka kwa wakulima.

Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dk. Stephan Ngailo, ndiye alitangaza mbolea hiyo mbadala mwishoni mwa wiki wakati akiwa kwenye ziara yake ya kutathmini hali ya upatikanaji wa mbolea katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema kulingana na matokeo ya utafiti uliofanywa na Kituo cha Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) walibuni mbolea nyingine mbadala ambayo ni NPC zinazofanya kazi sawa na mbolea nyingine.

"Mkulima akishindwa kumudu gharama za mbolea kama Dap na Urea zipo mbolea za samadi, Minjingu na NPC azitumie na atapata mavuno mengi tu, hivyo TARI imeshauri mbolea mbadala kama vile ASA zitumike," alisema Dk. Ngailo.

Hata hivyo, Dk. Ngailo alitumia fursa hiyo kueleza sababu za mbolea aina ya DAP na UREA kupanda bei katika kipindi hiki kwa maelezo kuwa hakuhusiani na tozo za kwenye miamala ya simu bali ni kutokana na ugonjwa wa corona hali iliyosababishwa na uzalishaji na uingizwaji wa mbolea hizo nchini.

Alisema asilimia 90 ya mbolea nchini inatoka nje, hivyo ugonjwa wa corona umechangia bei za mbolea kupanda, na kwamba hadi sasa serikali ina shehena ya kutosha ya mbolea na kuongeza kwamba msimu wa kilimo wakulima hawatapata shida.

"Mtakumbuka mwaka jana watu walikuwa (lockdown) uzalishaji ulisimama na kusababisha kuwapo na mahitaji makubwa ya wakulima vilevile, katika soko la dunia bei ikapanda kwa sababu Tanzania tunategemea mbolea kutoka nje tukawa waathirika, nawahakikishia msimu huu mbolea ipo ya kutosha," alisema Dk. Ngailo.

Baadhi ya wasambazaji wa mbolea katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini walisema wamejiandaa vyema kuwafikishia wakulima mbolea kwa wakati kabla ya msimu ujao wa kilimo kuanza Septemba mwaka huu.

Mmoja wao, Leonard Mpayo, alisema wana mbolea aina ya Urea tani 4000, Dap 200 na nyingine, hivyo wamejipanga kusambaza mbolea maeneo yote ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

# Mbarali yawapa neno wawekezaji

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, amewataka wawekezaji kufuata sheria na miongozo ya uwekezaji ikiwamo kushiriki shughuli mbalimbali za kijamii.

Miongoni mwa shughuli hizo ni ujenzi wa shule, vituo vya kutolea huduma za afya na uboreshaji wa miundombinu ya maji.

Mfune alitoa kauli hiyo juzi wakati wa ziara ya kamati ya ulinzi na usalama iliyofanyika kwenye kata za Chimala na Ilongo, na kusema kuwa wawekezaji wapya wa maghala na wenye viwanda vya kuchakata zao la mpunga wanapaswa kufuata na kuzingatia kanuni za uwekezaji sambamba na kujenga mahusiano mazuri na wananchi wanaozunguka maeneo hayo.

Alisema lengo la kuwatembelea wawekezaji wapya wanaojenga maghala pamoja na viwanda vya kuchakata zao la mpunga na kupata mipango yao wanavyowasaidia wakulima wa Mbarali.

Aidha, mkuu huyo wa wilaya aliwapongeza wawekeza kwa kuwekeza katika wilaya hiyo sambamba na kutoa huduma kwa wakulima pamoja na kuhifadhi mazao.

"Nawapongeza ndugu zangu kwa kuwekeza katika wilaya hii, lakini hii itawasaidia pia kuwa wanufaika wa uwekezaji huu mlioamua itasaidia wakulima kuhifadhi mazao yao ili yakipanda thamani muweze kuuza," alisema Mfune.

Hata hivyo, Mfune alisema siku zote wamekuwa wakitangaza maeneo ya uwekezaji yaliyopo wilayani hapa, hivyo ni vema wakulima wakatumia vizuri fursa hiyo na ambao hawajaziona ni muda mwafaka kuja wa kuwekeza katika maeneo yao.

"Siku zote tumekuwa tukitangaza maeneo ya uwekezaji yaliyopo wilayani hapa, niwasihi na wengine ambao hawajaona hizi fursa waje wawekeze," alisema Mkuu huyo wa Wilaya.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wawekezaji hao walimshukuru Mkuu wa Wilaya hiyo kwa kuwatembelea na kuwatia moyo, na kuahidi kuwasaidia wakulima pamoja na kushirikiana na jamii inayowazunguka.

Katika ziara hiyo ambayo mkuu wa wilaya aliongozana na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo, pia alitembelea ujenzi wa ghala la kuhifadhi mazao lililopo Kijiji cha Mengele kata ya Chimala linalomilikiwa na wawekezaji David na Neema Kiumba pamoja na ujenzi wa ghala la kuhifadhia mazao lililopo Kata ya Mahongole Kijiji cha Nsonyaga linalomilikiwa na kampuni ya Rahab Logistics.



# Asma Mwinyi Foundation yagawa taulo za kike

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANAFUNZI wa kike wa Shule ya Sekondari Tumbatu, wamesema wanahitaji elimu ya hedhi salama kwa sababu zana wanazotumia kipindi hicho ni za asili.

Waliyasema hayo baada ya kukabidhiwa taulo za kike na kupewa elimu ya matumizi ya taulo hizo na Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation. Walisema zana za asili wanazotumia kipindi cha hedhi husababisha kukosa masomo kwa muda kutokana na kushindwa kuhudhuria shule kwa ufanisi.

"Zana za asili tunazotumia wakati wa hedhi huwa zinavujisha hivyo inatulazimu tubadilishe kila baada ya muda, hutuwia vigumu kwenda shule wakati tupokuwa katika siku zetu za hedhi," alisema Harun Sheha Pandu, mwanafunzi wa kidato cha tatu.

Alisema wanapokuwa katika siku zao huona aibu kuhudhuria shule kwa sababu darasani kuna mchanganyiko wa wanafunzi wa kike na kiume na zana wanazotumia sio rafiki kwao ndiyo maana huamua kubaki nyumbani hadi hali itakapokua vizuri.

Alisema wasichana wa Kisiwa cha Tumbatu matumizi yao ni zana za asili wakati wanapoingia katika hedhi na matumizi ya taulo za kike ni mageni kwao.

Alisema wanahitaji elimu ya matumizi ya taulo za kike, pia msaada wa taulo hizo kwa sababu wazazi wao hawana uwezo wa kugharamia kila mwezi.

"Tunaipongeza sana Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation kwa msaada huu wa taulo za kike ambapo wametupatia za muda wa miezi mitatu, tuna imani kuwa sasa tutahudhuria shule kipindi chote na tutapoingia katika siku zetu za hedhi tutakuwa hatuna wasiwasi," alisema. Naye Sheha wa Tumbatu Jongowe, Miza Ali Sharif, alisema hedhi kwa wanafunzi wa kike ni moja ya changamoto kubwa na baadhi ya wanafunzi hushindwa kuhudhuria shule.

Alisema msaada huo utasaidia kuwawezesha kuhudhuria kikamilifu masomo yao bila ya kukosa katika kipindi chote.

Aliziomba taasisi zingine na watu wenye uwezo kuendelea kuwapatia msaada mbalimbali kwa sababu hali za kiuchumi za wananchi wa Kisiwa cha Tumbatu ni duni.

Akipokea mgao wa taulo hizo kutoka kwa Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Katibu Tawala wa wilaya ndogo ya Tumbatu, Khatib Habib Ali, alisema mgao huo umekuja kwa wakati muafaka kwa kuwa mahitaji ya taulo hizo ni makubwa ili kuwajengea uwezo zaidi wanafunzi wa kike kujiamini na kupata elimu katika kipindi chote hata wanapopata mabadiliko ya kimwili. Alisema mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha makundi yote yanapata elimu ambayo ni haki ya msingi kwa mujibu wa Katiba ikiwamo wanawake.

"Wilaya ndogo ya kisiwa cha Tumbatu tumefarajika sana na kupata mgao wa taulo za kike kwa wanafunzi wetu wa sekondari hatua ambayo itasaidia kuleta ufanisi na kasi ya mabadiliko ya sekta ya elimu," alisema.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, aliwataka wanafunzi hao kuzitumia vizuri kwa matumizi sahihi zaidi pale wanapokabiliwa na mabadiliko ya mwili ya kupata hedhi.

Alisema baadhi ya wanafunzi wanaokabiliwa na mabadiliko ya kuingia katika kipindi cha hedhi hushindwa kuhudhuria masomo hadi wanapokuwa salama na huchukua muda wa siku saba.

Alisema hali hiyo hurudisha nyuma maendeleo ya elimu kwa wanafunzi hao na wakati wao wakikosa masomo wenzao wa kiume wanaendelea kufaidika.

Jumla ya wanafunzi 500 wamapata mgao wa taulo hizo ambazo zitawawezesha kuendelea na masomo yao hata pale wanapokabiliwa na mabadiliko ya kimwili.



Wanafunzi wa kike wa Shule ya Sekondari Tumbatu wakifurahia msaada waliopewa wa taulo za kike ambazo zimetolewa na Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation pamoja na mwenyekiti wa taasisi hiyo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Mkuya awataka watumishi wizara yake kufikia malengo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya Salum, amewataka wafanyakazi wa wizara hiyo kutekeleza vyema majukumu yao ili kufikia lengo lililokusudiwa na serikali la kutoa huduma bora kwa wananchi.

Aliyasema hayo wakati wa makabidhiano ya ofisi kwa makatibu wakuu na kuwataka kushirikiana katika utendaji wa kazi na kuwakaribisha na kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Alisema mwelekeo wa kazi katika wizara hiyo unakwenda vizuri na aliwasisitiza kuwa naye karibu katibu mpya katika kutekeleza majukumu ya serikali na kila mfanyakazi kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Alimshukuru katibu aliyebadilishiwa wizara kwa kufanya kazi zake vizuri na kumuomba anakokwenda akatimize wajibu na uimara wake.

Naye Katibu Mkuu Kazi na Uwezeshaji, Khadija Khamis Rajab, alisema kwa muda aliofanya kazi katika wizara hiyo amerekebisha mambo mengi kwa ushirikiano alioupata baina yake na wafanyakazi wenzake.

Miongoni mwa marekebisho hayo ni kupunguza baadhi ya madeni ya wafanyakazi ikiwamo mrundikano wa fedha za likizo na mambo mengine.

Kwa upande wake Katibu Mkuu mpya wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Omar Dadi Shajack, aliahidi kufanya kazi kwa ushirikiano ili majukumu ya kazi yaweze kuendelea ikiwamo uwajibikaji kwa kila mmoja.

# Vyama vyaonywa shinikizo la Katiba mpya

**Na Mwandishi Wetu**

VYAMA vya siasa nchini vimetakiwa kuacha kutoa mashinikizo kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Samia Suluhu Hassan, ikiwamo madai ya Katiba mpya na kutishia kufanya maandamano nchi nzima.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa nchini, Juma Ali Khatib, alisema huu ni wakati wa vyama vya siasa kutoa ushirikiano kwa Rais Samia Suluhu Hassan, katika kuimarisha uchumi na kuwaunganisha wananchi wa Tanzania kulingana na ahadi alizozitoa kwa wapiga kura. Khatib alisema msimamo wa viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kudai Katiba mpya na kutishia kufanya maandamano nchi nzima hauna nafasi kwa sasa kwa sababu tayari Rais Samia ameonyesha utayari wake wa ushirikiano na kufanya kazi na makundi mbalimbali nchini.

Alisema Rais Samia tangu aliposhika nafasi ya urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa akifanya kazi vizuri kwa kuwashirikisha wananchi mbalimbali huku akitoa ahadi za kuyaunganisha makundi mbalimbali katika siasa na ujenzi wa taifa.

Alisema kauli zake za kuwaunganisha wananchi kupitia makundi zimejenga matumaini makubwa kwa wananchi wa Tanzania wenye rika tofauti kuanzia wasomi, wanasiasa na wafanyabiashara wadogo.

Alisema tabia inayofanywa na uongozi wa chama hicho cha upinzani ikiwamo mabadiliko haraka ya Katiba si jambo zuri na kila jambo linafanyika kwa wakati wake.

"Nazungumza nikiwa Mwenyekiti wa Baraza la Umoja wa Vyama vya Siasa nchini...huu sio wakati muafaka wa kutoa shinikizo kwa Rais Samia kufanyika kwa mabadiliko ya Katiba kwani rais kwa nyakati tofauti ametoa ahadi zake za kuyashirikisha makundi mbalimbali nchini ikiwamo vyama vya siasa katika uongozi wa nchi na matokeo yake tumeyaona kwa baadhi ya uteuzi wa viongozi," alisema.

Khatib ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha ADA-TADEA na mjumbe wa kuteuliwa Baraza la Wawakilishi na uteuzi wa Rais ametoa mfano katika kutekeleza ahadi za rais kwa kumteua aliyekuwa mgombea wa urais kupitia chama cha upinzani cha ADC, Queen Sendiga, kuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa.

Pia alisema wakati Rais Samia akishika madaraka amekabidhiwa na majukumu makubwa ya kutekeleza na kusimamia miradi ya kimkakati ambayo imelenga zaidi kuinua uchumi na kuihakikishia Tanzania kupiga hatua kubwa ya maendeleo kuwa miongoni mwa nchi zinazoendelea.

## Bodi REA yaagiza makandarasi kasi

**Na Veronica Simba**

WAJUMBE wa Bodi ya Nishati Vijijini, wametembelea Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme Ifakara, mkoani Morogoro na kuwaagiza makandarasi kuukamilisha ndani ya muda uliopangwa.

Wajumbe hao wakiongozwa na Mwenyekiti wake, Wakili Julius Kalolo, waliambatana na wataalamu kadhaa kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA), akiwamo Mkurugenzi Mkuu, Mhandisi Amos Maganga pamoja na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya ziara hiyo, Wakili Kalolo alisema bodi imeridhika na mpango mkakati uliowasilishwa kwao na mkandarasi anayejenga kituo hicho, Kampuni ya AEE kutoka Hispania.

Kalolo alisema bodi ililazimika kutembelea mradi huo ili kujionea maendeleo pamoja na kuzungumza na makandarasi baada ya kupata taarifa za kusuasua kwake.

"Kulikuwa na tatizo la ucheleweshaji ambalo mwanzoni lilitokana na tatizo la corona, hivyo baadhi ya vifaa vilivyotakiwa kuletwa havikuletwa kwa wakati," alisema Kalolo.

Alisema bodi hiyo ilifanya ziara katika mradi husika Januari, mwaka huu na kutoa maelekezo kuwa udhaifu uliopo ufanyiwe kazi na ndiyo lengo la kutembelea eneo hilo tena ili kujiridhisha endapo maelekezo yao yalizingatiwa.

Alisema pamoja na bodi kuridhishwa na mpango mkakati uliohuishwa, bado imebaini upungufu wa wafanyakazi na hivyo imeelekeza idadi yao iongezwe ili wafanye kazi kwa kasi zaidi na viwango kama ilivyokusudiwa.

Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Maganga, alibainisha kuwa wanaimani kuwa endapo makandarasi watatekeleza kikamilifu mpango mkakati waliouhuisha, hakuna shaka kuwa mradi utakamilika ndani ya wakati uliopangwa.

Aliongeza kuwa, REA imejipanga kufuatilia utekelezaji wa mradi huo hatua kwa hatua ili kuhakikisha unakamilika kwa wakati na viwango vya juu, ili uwanufaishe wananchi waliokusudiwa.

Mkandarasi anayejenga kituo hicho, Kampuni ya AEE, Francis Kahumbi, alisema watatekeleza maelekezo yote yaliyotolewa na bodi ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati.

Meneja Mradi Ifakara kutoka TANESCO, Mhandisi Didas Lyamuya, alisema umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni ujenzi wa kituo cha upoza umeme pamoja na usambazaji umeme katika vijiji nane na vitongoji saba.



Abiria wakijaribu kuingia katika daladala, kituo cha Mbezi Mwisho jijini Dra es Salaam juzi, huku wengine wakiwa hawajavaa barakoa kama tahadhari ya kujikinga na corona. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Sendiga kuwabana wasiotunza watoto

**Na Francis Godwin, IRINGA**

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, ameagiza viongozi wa kata na vijiji vyote wilayani humu kuwafuatilia na kuchukua hatua kali kwa wazazi wote wanaoendekeza ulevi na kutowajali watoto wao.

Amesema hali hiyo inachangia ongezeko la udumavu wa asilimia 47 kwa watoto mkoani Iringa.

Katika hotuba yake ya ufunguzi wa kituo cha Utengamavu kwa watoto wenye ulemavu mjini Iringa kilichojengwa na Shrika la Call Afrika katika eneo la Frelimo mjini Iringa juzi, Sendiga aliyewakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, alisema lazima mabaraza ya madiwani kutunga sheria ndogo ndogo zitakazowabana wazazi hao wasio wajibika kwa watoto wao.

"Wapo baadhi ya wazazi kazi yao ni ulevi na hawana habari na familia zao, jambo ambalo limekuwa likiongeza kasi ya udumavu ndani ya Wilaya ya Iringa na serikali ya wilaya na mkoa haipo tayari kuona kasi ya udumavu inaendelea kwa sababu tu ya wazazi wachache wasiotimiza wajibu wao kwa familia," alisema.

Alisema haiwezekani raia wa Italia wakajitolea kusaidia tatizo la udumavu na ulemavu kwa watoto mkoani Iringa huku wazazi wachache wa mkoa wa Iringa wakipuuza na kuendekeza ulevi usio na tija katika familia zao.

Hivyo alisema ni lazima kujipanga kuweka sheria ndogo ndogo zitakazowalinda watoto dhidi ya udumavu, na kwamba pia sheria zitakazowabana wazazi wasiopenda kuwajibika kwa watoto wao kiafya.

Alisema kuwa kila mzazi ana wajibu wa kumtunza mtoto wake basdala ya kuendekeza ulevi, na kwamba kupitia sheria hizo zitakazotungwa zitawabana wazazi wenye tabia hizo kuwajibika kwa familia zao na atakaposhindwa kuwajibika basi sheria ichukue mkondo wake.

Mbunge wa Iringa Mjini, Jesca Msambatavangu na Naibu Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Kenyatta Likotiko, waliiomba jamii ya mji wa Iringa kutumia vema kituo hicho badala ya kufanya hujuma ama kutopeleka watoto wenye ulemavu kupata tiba ya ulemavu.

## TADB yakosha viongozi mila kuwezesha wakulima wazawa

**Na Mwandishi Wetu, MBEYA**

VIONGOZI wa kimila wa Mkoa wa Mbeya wameipongeza Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa kuwawezesha wakulima na wawekezaji wazawa nchini. Viongozi hawa walisema hayo wakati wa ziara maalum ya kutembelea Kiwanda cha Raphael Group Ltd., leo, katika Wilaya ya Uyole.

Mkuu wa Machifu wa Mbeya Jiji na Vijijini, Chifu wa kabila la Wasafwa, Rodrick Mwashinga, aliipongeza TADB kwa uwekezaji wake katika kampuni ya Raphael Group Ltd., moja ya kampuni inayoongoza Nyanda za Juu Kusini katika kuzalisha, kuchakata na kuuza nafaka.

"Ninapenda kuwashukuru sana TADB kwa kuwawezesha wakulima na wawekezaji wazawa katika mkoa huu. Hii inadhihirisha imani iliyonayo TADB kwa wawekezaji wa ndani na waliotoka katika jamii zetu wenyewe," alisema Chifu Mwashinga.

Aliongeza: "Uwekezaji huu wa TADB pia inadhihirisha nia yao ya kusaidia jamii katika kuleta maendeleo ya kiuchumi kupitia shughuli ya kilimo...hivyo, napenda kutoa wito kwa benki hii iendelee kupanua wigo wa utoaji wake wa mikopo kwa wakulima na wawekezaji wazawa ili kuweza kujenga viwanda kama hivi vingi zaidi, kuongeza ajira, kuleta uhakika wa masoko wa mazao ya wakulima, na kuchagiza maendeleo ya mkoa na uchumi wa nchi kwa ujumla wake."

Akizungumzia uwekezaji wa TADB katika kampuni ya Raphael Group Ltd., Meneja wa Kanda wa Nyanda za Juu Kusini kutoka benki hiyo, Alphonce Mukoki, alisema benki hiyo imeiwezesha kampuni ya Raphael Group kupata mashine ya kisasa ya kuchakata tani 80 ya mpunga kwa siku, mashine ya kukausha mpunga na mashine ya uhakiki na utengaji wa rangi ya mchele. Pamoja na hayo, benki pia imeipatia kampuni hiyo mtaji wa uendeshaji kwa ajili ya kununua mpunga na maharage kutoka kwa wakulima wadogo zaidi ya 13,000 Mbeya na mikoa ya jirani.

Mukoki pia alisisitiza nia ya benki hiyo katika kuwawezesha wakulima na wawekezaji wazawa katika kuchagiza mageuzi ya kilimo na kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini.

"Malengo yetu kama benki ya maendeleo ni kuwawezesha wakulima na wawekezaji wazawa na teknolojia ya kisasa, pamoja na mtaji wa kuinua sio tu biashara zao bali pia kuleta manufaa kwa minyororo ya thamani husika," alisema Mukoki.

Kutokana na taarifa kutoka TADB, hadi Juni mwaka huu, benki hiyo imekwisha wekeza zaidi ya shilingi bilioni 30 katika Nyanda za Juu Kusini, ikiwamo mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe, Ruvuma na Songwe, katika minyororo ya thamani 18, ikiongozwa na zao la mpunga, kakao, mahindi na kahawa.

Meneja Mkuu wa Raphael Group Ltd., Lazaro Mwakipesile, alisema nia ya ziara ya viongozi hao wa kimila ilikuwa ni kuelimisha jamii juu ya ushirikiano katika ya TADB na kampuni hiyo, pamoja na kushuhudia moja kwa moja shughuli ya kiwanda hicho ya kuzalisha, kusindika na kuuza nafaka.

"Ushirikiano katika uwekezaji huu kiuhakika utatangaza mkoa wa Mbeya na Tanzania kwa ujumla kama kitovu cha kuzalisha, kuchakata na kuuza mpunga," alisema Shitambala.

Raphael Group Ltd., ni moja ya kampuni inayoongoza Nyanda za Juu Kusini katika kuchakata na kuuza nafaka aina sita tofauti. Zao la mpunga linachukua asilimia kubwa (asilimia 50) ya biashara ya kuchakata ya kiwanda hicho, ikifuatia na maharage (asilimia 20), karanga (asilimia 10), na mahindi (asilimia 5).

HABARI KIMATAIFA

# Mapigano yazuka makundi hasimu ya Riek Machar

**Juba, SUDAN KUSINI**

MAPIGANO makali yalizuka Jumamosi kati ya makundi hasimu ya Makamu Rais wa Sudan Kusini, Riek Machar wa SPLA-IO, msemaji wake wa jeshi amesema katika taarifa.

Mapambano yalizuka baada ya mahasimu wa Machar kutangaza wiki hii kuwa wamemwondoa kama mkuu wa chama na kwenye uongozi wa kijeshi wa chama hicho.

Majeshi yalikuwa yakiongozwa na jenerali hasimu katika chama, Simon Gatwech Dual, ambaye alianzisha shambulizi kwa watu wa Machar, ambao walichukizwa na wachokozi, msemaji Col. Lam Paul Gabrie alisema.

Jeshi la Machar la SPLA-IO limewaua mameja jenerali wawili na wengine zaidi ya 27 wanajeshi adui, wakati wao wamepoteza watu watatu tu, aliongezea.

Mapigano hayakuweza kuthibitishwa na vyanzo huru na hakuna majibu ya haraka kutoka upande wa Gatwech Dual.

Viongozi wa tawi la kijeshi la Machar la SPLM/A-IO walisema walimwondoa kiongozi ambaye aliwahi kuwa muasi na hivi sasa ni mwanasiasa kwa kushindwa kuwakilisha maslahi yao.

Mapigano yanaweza kuweka shinikizo kwa makubaliano tete ya mwaka 2018 ya kushirikiana madarakani kati ya Machar na hasimu wake wa zamani Rais Salva Kiir.

Washirika wa Machari, Ijumaa walitupilia mbali kuondolewa kwake madarakani na kusema kuwa ni mapinduzi yaliyofeli na kusisitiza kuwa bado ana udhibiti kamili katika chama.

Machar mwenyewe wiki hii aliwashutumu waharibifu wa amani kwa kufanya njama za kumwondoa mamlakani.

Kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 68 amenusurika katika miaka kadhaa ya vita vya msituni, majaribio ya kuuawa na kuishi muda mrefu uhamishoni, amehudumu kama makamu wa rais pamoja na Kiir katika serikali ya kwanza baada ya uhuru kutoka Sudan mwaka 2011.

Viongozi hao wawili baadaye walikosana na Machar alifukuzwa kazi miaka miwili baadaye.

Wanajeshi watiifu kwa kila upande walishirikiana silaha, na Sudan Kusini ilitumbukia katika miaka mitano ya vita vya wenyewe kwa wenyewe.

*VOA*



Darasa likiwa limeharibiwa na shambulizi la angani jijini Lashkar Gah Jimbo la Helmand, Kusini mwa Kabul nchini Afghanistan, huku shambulio hilo likiathiri kituo cha afya na shule, jana. **PICHA: AP**

# Saudia yafungua hija ndogo kwa waliochanjwa corona

**Makka, SAUDI ARABIA**

SAUDI Arabia itafungua tena hija ya Omra (hija ndogo) kwenda Makka kwa mahujaji kutoka nchi za kigeni waliopewa chanjo dhidi ya Covid-19, shirika la habari la Saudi Arabia limeripoti jana.

Mamlaka ya Saudia itaanza kuidhinisha maombi ya kuingia kuanzia leo, shirika hilo lilisema.

Mipaka ya nchi hiyo ilifungwa miezi 18 iliyopita kutokana na janga hilo hatari.

Hija ndogo (Umrah), ambayo ni tofauti na Hija kubwa, inaweza kufanywa kwa mwaka mzima, kawaida huvutia mamilioni ya wageni kutoka kote duniani kila mwaka.

Janga la Covid-19 limevuruga sana ibada ya Hija na Umrah, vyanzo muhimu vya mapato kwa nchi hii ya kifalme ambavyo huingiza dola bilioni 12 kwa mwaka.

Hadi sasa, ni mahujaji waliopewa chanjo tu wanaoishi Saudi Arabia ndio waliokubaliwa kufanya Hija ndogo (Umrah).

Mahujaji wa kigeni wanaotaka kusafiri kwenda Makka pia watahitaji kupatiwa chanjo na kibali kinachotambuliwa na Saudi Arabia, na kuzingatia sheria za karantini, shirika la habari la Saudi limeongeza, likinukuu wizara yenye dhamana ya Hija.

Saudi Arabia imewekeza mabilioni katika tasnia ya utalii katika miaka ya hivi karibuni ili kubadilisha uchumi wake wa mafuta.

Kwa muda mrefu, nchi hii ilitoa visa vya kwanza vya watalii mwaka 2019.

Kati ya mwezi Septemba 2019 na kufungwa kwa mipaka mwezi Machi 2020, ilitoa visa 400,000 vya watalii.

Tangu kuzuka kwa mgogoro wa kiafya, Saudi Arabia imerekodi zaidi ya visa 5,321,000 vya maambukizi na zaidi ya vifo 8,300.

Serikali iliharakisha kampeni ya chanjo mapema Agosti, kwa lengo la kufufua utalii na kuandaa hafla za michezo na maonyesho.

Chanjo sasa ni lazima kuingia katika vituo vya umma na vya kibinafsi, pamoja na shule na maeneo ya burudani, na pia kutumia usafiri wa umma.

*RFI*

# Mamia wafanyakazi ujenzi waandamana Ujerumani

**Bonn, UJERUMANI**

MAMIA ya wafanyakazi katika sekta ya ujenzi Ujerumani, wamefanya maandamano katika maeneo tofauti ya taifa hilo kushinikiza malipo bora na mazingira mazuri ya kufanyia kazi.

Kwa mujibu wa Chama cha Wafanyakazi wa Sekta ya Ujenzi IG BAU, mamia ya wafanyakazi kutoka katika majimbo kadhaa ya shirikisho walishiriki maandamano hayo katika miji tofauti.

Msemaji wa chama hicho cha wafanyakazi alieleza kwamba, pamoja na kufanyika duru tatu tofauti za mazungumzo, waajiri wameshindwa kutoa kiwango kinachokubalika cha nyongeza ya mishahara na posho kwa wafanyakazi hao wanao safiri kwa muda mrefu kwenda katika maeneo ya ujenzi.

Mbali na posho ya usafiri, IG Bau inadai nyongeza ya asilimia 5.3 ya mishahara na usawa wa kima cha mishahara kwa wafanyakazi wa upande wa Mashariki na Magharibi mwa Ujerumani.

**DW**




# AGUERO
## HANA MPANGO KUONDOKA BARCELONA

**BARCELONA, Hispania**

SERGIO Aguero hatoondoka Barcelona msimu huu wa majira ya joto kwani malengo yake ni kupata mafanikio na klabu hiyo.

Mshambuliaji huyo raia wa Argentina amedhamiria kucheza hapo Camp Nou licha ya kuwa sasa anajua kwamba, hatakuwa na Lionel Messi ambaye ni rafiki yake.

Amewasili kwenye klabu na hafikirii mabadiliko mengine, licha ya ripoti kwamba kuondoka kwa Messi kunaweza kusababisha kuyumba kwa klabu hiyo.

"Wacha tuamini tutacheza pamoja," Aguero alisema baada ya kujiunga na uhamisho wa bure kutoka Manchester City.

"Yeye ni vizuri kucheza naye na inanipa kiburi kufanya hivyo. Ninamjua sana na nadhani atabaki."

Aguero alijiunga na 'Wakatalunya' hao mapema msimu huu wa majira ya joto, baada ya mkataba wake wa City kumalizika Juni 30, mwaka huu.

Moja ya sababu za chaguo lake kuhamia Barcelona ilikuwa ni kucheza na rafiki yake wa karibu Messi, ambaye sasa haitatokea.

Wawili hawa hawawezi kutenganishwa katika kiwango cha kimataifa na Argentina, lakini sasa watacheza kwa pande tofauti za klabu, wakiwa hawajawahi hata kupata nafasi ya kufanya mazoezi pamoja huko Catalunya.

Kupitia ukurasa wake wa Istagram, Aguero ameandika kwamba, ataendelea kucheza Barcelona licha ya rafiki yake kuondoka.

"Nilikuja hapa nikiwa na nia ya kufanya vizuri na kucheza na rafiki yangu Lionel Messi, lakini sasa sitakuwa naye, lakini siwezi kuondoka."

# PARTEY NJE WIKI TATU ARSENAL

**LONDON, England**

ARSENAL wamebainisha kuwa kiungo wao, Thomas Partey, anatarajiwa kukaa nje kwa wiki tatu kutokana na jeraha la kifundo cha mguu.



Mchezaji huyo wa zamani wa Atletico Madrid, alipata jeraha wakati alipokabana na Ruben Loftus-Cheek katika mechi ya wikendi iliyopita dhidi ya Chelsea.

Partey alikosa michezo 17 msimu uliopita ukiwa ni msimu wake wa kwanza Arsenal kwa sababu ya shida ya majeraha, na 'Washikabunduki' hao sasa wamethibitisha kuwa matarajio ya kucheza tena mwezi huu ni duni.

Taarifa ya Arsenal kupitia tovuti yake ilisema: "Thomas alipata jeraha kwenye kifundo cha mguu wake wa kulia wakati wa mechi ya kirafiki dhidi ya Chelsea Jumapili iliyopita. Thomas anaendelea kufanyiwa uchunguzi na anatarajiwa kurejea mazoezini angalau wiki tatu zijazo."

Partey ambaye alishiriki mechi 33 za mashindano yote akiwa na Arsenal msimu uliopita, ameungana na Eddie Nketiah (kifundo cha mguu) na Gabriel Magalhaes (goti) kuuguza majeraha kabla ya kurejea dimbani.

Washikabunduki watafungua kampeni yao ya Ligi Kuu England dhidi ya Brentford Ijumaa ijayo kabla ya mechi dhidi ya Chelsea na Manchester City baadaye mwezi huu.

# JORGINHO AFURAHIA TETESI KUTUA LUKAKU

**LONDON, England**

KIUNGO wa Chelsea, Jorginho ametoa mawazo yake juu ya tetesi za uhamisho wa mshambuliaji wa Inter Milan, Romelu Lukaku kutua katika klabu hiyo ambayo amewahi kuitumikia miaka 10 iliyopita.



Chelsea wamekubaliana kwa maneno na Inter Milan juu ya uhamisho wa mshambuliaji huyo ambao utamrudisha darajani kwa dau linalotarajiwa kuwa pauni milioni 97.5

Akihojiwa juu ya mazungumzo ya uhamisho na TNT Sports, kiungo wa Chelsea Jorginho amesema: "Mchezaji kama Lukaku, ambaye amekuwa na msimu mzuri na kuwa bingwa nchini Italia, hakika ni mchezaji ambaye anaweza kutusaidia sana.

"Mtu yeyote anayekuja kutusaidia atakuwa na thamani. Wacha tuone nini kitakotokea baadaye."

Lukaku amefunga mabao 64 katika mechi 95 ambazo ameichezea klabu ya Inter Milan tangu alipojiunga nao.



# SILVA
## ATAKA KUONDOKA CITY

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amethibitisha kuwa Bernardo Silva anataka kuondoka klabuni hapo.

Kiungo huyo raia wa Ureno anataka kuondoka Man City msimu huu wa majira ya joto na anapenda kucheza Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

City inatarajiwa kukubali matakwa ya Silva iwapo tathmini italingana na kiwango kinachodaiwa kushuka cha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, baada ya Jack Grealish kusajiliwa kwa pauni milioni 100 kutoka Aston Villa.

Barcelona haionyeshi uwezekano wa kumudu pauni za milioni 45 inazotaka City, lakini imepata ahueni baada ya Lionel Messi aliyekuwa akilipwa kiasi kikubwa cha fedha kuondoka.

Silva, aliyejiunga na Man City mwaka 2017 kwa pauni milioni 43 akicheza mechi 45 msimu uliopita, aliisaidia kushinda Kombe la Ligi Kuu England na Carabao.

# MESSI KUZUIA
## USAJILI WA POGBA

**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain imeripotiwa kuwa karibu na usajili wa Lionel Messi, bila shaka wababe hao wa Ufaransa watapoteza nia yao ya kumsajili Paul Pogba wa Manchester United.

Baada ya tangazo la Barcelona Alhamisi usiku juu ya kuachana rasmi na suala la mkataba mpya wa Messi, PSG wameweka wazi nia yao na wanafanya jitihada kukamilisha mpango wa kumsajili nyota huyo wa Argentina.

Awali, PSG ya Mauricio Pochettino ilikuwa ikihusishwa sana na Pogba, ambaye amebakiza chini ya mwaka mmoja kukamilisha mkataba wake wa sasa na mabingwa hao mara 20 wa England.

Laikini kwa mujibu wa ESPN, kuwasili kwa Messi huko Paris kutaathiri nia ya PSG kumsajili nyota wa Man United Paul Pogba, kwani klabu haitaweza kumudu mikataba yote miwili kwenye soko la sasa.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa sasa anaweza kuamua kumalizia mkataba wake huko Old Trafford kabla ya kuhama klabu hiyo kama mchezaji huru msimu ujao wa majira ya joto.

Lakini Man United bado inafikiriwa kuwa na matumaini ya kumsainisha mkataba mpya mshindi huyo wa Kombe la Dunia, baada ya kupanua kikosi chao kwa kuwaongeza Jadon Sancho na Raphael Varane kabla ya msimu mpya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, hivi sasa anafanya mazoezi na wachezaji wenzake wa 'Mashetani Wekundu' hao kabla ya msimu mpya wa 2021-22 kuanza.




# WAKALA ASHINIKIZA
## UHAMISHO WA CAMAVINGA

**PARIS, Ufaransa**

WAKALA wa nyota wa Rennes, Eduardo Camavinga, ameripotiwa kushinikiza kijana huyo kukamilisha uhamisho wa kwenda Manchester United msimu huu wa majira ya joto.

Camavinga aliibuka kuwa nyota muhimu na 'Les Rouge' hao akiwa na umri wa miaka 18, lakini kwa sasa anatarajia kuwa mchezaji huru mwaka 2022.

Baada ya mazungumzo juu ya mkataba mpya kushindwa kuzaa matunda hadi sasa, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Rennes, Florian Maurice, amethibitisha kuwa Camavinga atauzwa msimu huu wa majira ya joto ikiwa atapinga kuongeza mkataba wake.



Man United inaaminika ilimtambua kijana huyo kama mbadala wa Paul Pogba, na kwa mujibu wa mwandishi wa habari wa Ufaransa, Mohamed Bouhafsi, wakala wa Camavinga, Jonathan Barnett anatarajia mafanikio ya uhamisho wa kwenda Old Trafford kwa mteja wake.

Hata hivyo, Bouhafsi ameongeza kuwa Camavinga bado anatamani kuhamia Paris Saint-Germain, wakati inaaminika pia kuwa kuna nia ya kutoka klabu za LaLiga.

Mchezaji huyo wa Ufaransa tayari ameshacheza mechi 82 kwa Rennes kwenye mashindano yote, akifunga mabao mawili na kusaidia mengine matano kwa wakati huo.

HABARI MICHEZO

## KWA UFUPI

**POCHETTINO NA MESSI PSG**
KOCHA wa PSG, Mauricio Pochettino, amethibitisha kuwa mawasiliano yamefanyika kuhusu uhamisho huu wa Lionel Messi mwenye umri wa miaka 34, ili kujiunga na miamba hao wa Ligue 1. ***(ESPN)***

**MESSI AITAKA MAN CITY**
LIONEL Messi mwenyewe anaelezwa kuwa chaguo lake la kwanza ni kuona anaungana tena na kocha, Pep Guardiola akiwa pale Manchester City. ***(Mail)***

**MADRID WAMZUIA ODEGAARD**
REAL Madrid wamezuia uhamisho wa kiungo wa kati wa Norway, Martin Odegaard mwenye umri wa miaka 22, kwenda Arsenal baada ya Toni Kroos kupata jeraha. ***(AS,via Team Talk)***

**AGUERO KUONDOKA BARCA**
MSHAMBULIAJI wa Argentina, Sergio Aguero, aliyejiunga na Barcelona Mei mwaka huu baada ya kuondoka Manchester City, anaelezwa anataka kuondoka kwenye klabu hiyo ya Catalunya baada ya kutangazwa kuwa rafiki yake wa karibu Lionel Messi hatasalia hapo Nou Camp. ***(Betevein Catalan)***

**CHELSEA BADO NA INTER**
CHELSEA wameendelea kuwa na uhakika wa kuingia makubaliano na Inter Milan kwa ajili ya kumsajili tena Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 28, huku kocha Thomas Tuchel akitarajia kumaliza mchakato wa uhamisho kabla ya kuanza kwa msimu mpya. ***(Standard)***

**NEYMAR KUMPA JEZI MESSI**
MSHAMBULIAJI wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 29, amempa ofa ya jezi yake namba 10 Lionel Messi kama atatua PSG. ***(RMC Sport)***

**BARCA KWA SANCHEZ**
BARCELONA wamekubaliana na kiungo wa kati wa Ureno, Renato Sanches mwenye umri wa miaka 23, lakini hawajakubaliana suala la ada na klabu yake ya Lille. ***(Le10 Sport)***

**WEST HAM KWA MILENKOVIC**
WEST Ham wamesalia kwenye mazungumzo na Fiorentina kuhusu dili la pauni milioni 14 kwa ajili ya mlinzi, Nikola Milenkovic mwenye umri wa miaka 23, lakini watakabiliwa na ushindani kutoka Juventus. ***(Mail)***

**CALETA-CAR AWANIWA**
WEST Ham pia inawania kumsajili mlinzi wa Marseille, Duje Caleta-Car mwenye umri wa miaka 24, baada ya nyota huyo kukataa ofa yao msimu wa majira ya joto uliopita. ***(L'Equipe)***

**SARGENT HUYO NORWICH**
MSHAMBULIAJI wa Marekani, Josh Sargent mwenye umri wa miaka 21, yuko karibu kumaliza hatua za uhamisho kuelekea Norwich City akitokea Werder Bremen. ***(Goal)***

**SOUTHAMPTON YAKATAA DAU**
KLABU ya Southampton imekataa dau la pauni milioni 25 kutoka kwa Aston Villa kwa ajili ya kumuuza James Ward-Prowse mwenye umri wa miaka 26, na hawana nia ya kumuuza kiungo huyo wa kati msimu huu.***( Football Insider)***

**CHELSEA YAMTAKA DE LIGT**
CHELSEA inamtaka mlinzi wa Juventus, Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 21, na wanaweza kutoa ofa ya pauni milioni 50 na mshambuliaji Timo Werner mwenye umri wa miaka 25. Hata hivyo, Juve wanamtaka zaidi kiungo wa kati Muitaliano Jorginho mwenye umri wa miaka 29, sambamba na kitita cha fedha. ***(Calciomercatoweb)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LUKAKU, CHELSEA SASA NI RASMI KIMEELEWEKA

●●●Amefurahishwa sana na dili hili na aliiomba Inter kuondoa jina lake katika mechi ya...

**LONDON, ENGLAND**

CHELSEA imekubaliana na Inter Milan kwa ada ya euro milioni 115 kwa ajili ya usajili wa Romelu Lukaku, kwa mujibu wa 90min.com.

Raia huyo wa Ubelgiji aliiomba Inter kuondoa jina lake kwenye kikosi cha mechi ya kirafiki dhidi ya Parma jana Jumapili ili aweze kukamilisha mpango wake wa kurudi tena Stamford Bridge.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Lukaku mwenyewe ameshafikia makubaliano binafsi na klabu hiyo na atakuwa mchezaji anayelipwa mshahara mkubwa zaidi.

Ada hiyo ya euro milioni 115 imefikiwa baada ya pande zote mbili kukubaliana kuhusu uhamisho wa mchezaji huyo.

Ada hiyo ya Lukaku ambayo ni sawa na pauni milioni 97.5, itamfanya kuwa mchezaji wa pili ghali zaidi katika historia ya soka la Uingereza baada ya Jack Grealish, ambaye ameigharimu Manchester City pauni milioni 100.

Chanzo kilicho karibu na Lukaku kimethibitisha kuwa ni wazi kwamba, anaondoka jijini Milan kuelekea London.

"Amefurahishwa sana na dili hili na anajua kwamba, Roman Abramovich amefanya msukumo mkubwa na sasa anataka kumuonyesha yeye na Chelsea nini anachoweza kufanya.

"Kila mmoja anajua bado alikuwa hajamaliza kazi aliyoianza kule Stamford Bridge."

Mapema Ijumaa, ripoti zilidai kwamba, Chelsea inapanga kupelekea ofa ya pili kwa ajili ya kumsajili Lukaku.

Ofa yao ya kwanza ilikataliwa na hivyo, wakaamua kurudi kwa mara ya pili na kufikia makubaliano ya kumnunua mchezaji huyo.

Inter imelazimika kumuuza mchezaji huyo kutokana na kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na mlipuko wa virusi vya corona na hivyo hali ya kiuchumi ya klabu hiyo kwa sasa ni mbaya.

Baada ya kutwaa ubingwa wake wa kwanza wa Ligi Kuu kwa kipindi cha miaka 10, Inter iliachana na kocha wake, Antonio Conte na pia ikamuuza Achraf Hakimi kwenda PSG.

HABARI MICHEZO

# NABI KUAMUA HATIMA YA AMBUNDO, UKONDE

**Na Adam Fungamwango**

HATIMA ya wachezaji Dickson Ambundo na Jimmy Ukonde kusajiliwa katika kikosi cha Yanga, sasa ipo mikononi mwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nasreddine Nabi.

Kocha wa Makipa wa Yanga, Razack Siwa, amesema kuwa uamuzi wa kusajiliwa wachezaji hao atakuwa nao kocha huyo mkuu, baada ya kuonekana kucheza mechi tatu za michuano ya Kombe la Kagame.

Siwa ambaye alisimama kama kocha kwenye michuano hiyo na kikosi cha Yanga, kwa upande wake, alisema wachezaji wote wawili walicheza vema, lakini yeye si mwamuzi wa mwisho.

"Kwa upande wangu, wachezaji wote wamecheza vizuri. Ukonde na Ambundo pia ni wachezaji wazuri, uamuzi sasa ni kwa kocha mkuu. Mimi nitakachofanya nitampa ripoti. Na ripoti yangu itasema tu kuwa ni wachezaji wazuri, lakini yeye ndiye ataamua, hivyo ikiwezekana Mungu akipenda tunaweza kuwa nao kwenye kikosi," alisema kocha huyo.

Wakati Siwa akisema hayo, baadhi ya wanachama na mashabiki wa Yanga wanadai kuwa kati ya hao wawili, Ambundo ameonekana kuwa anafaa kusajiliwa, huku wakiwa wamegawanyika kwa Ukonde, baadhi wakisema ni mchezaji wa kawaida sana, wengine wakitaka apewe muda.

Kuhusu wachezaji wa kikosi cha U-20 waliocheza michuano hiyo, Siwa alisema kuna baadhi atapendekeza pia waingizwe kwenye kikosi cha kwanza kwa sababu wameonyesha uwezo mkubwa.

Yanga imetolewa kwenye michuano ya Kombe la Kagame, baada ya kushika nafasi ya tatu, lakini baadhi ya wachezaji walioikuwa katika majaribio wakionyesha uwezo mkubwa.

Naye beki wa timu hiyo, Abdallah Shaibu 'Ninja', alisema kuwa hawakufanya vema kwenye michuano hiyo kwa sababu wamekutana na timu kutoka nje ya nchi, lakini wamejifunza kitu.

"Unajua unakutana na timu kutoka nje ya nchi ndiyo maana kumekuwa na ugumu. Lakini tumejifunza kitu sisi wachezaji na hata makocha wamejifunza kitu na tutarekebisha upungufu, lakini kikosi bado kipo vizuri tu," alisema.

TUZO...




Meneja Mwandamizi wa Huduma za Wateja Maalum na Diaspora Benki ya CRDB, Gibson Mlaseko (kulia), akimkabidhi tuzo mmoja wa washindi wa mashindano ya mchezo wa gofu kwa taasisi, Joseph Tango. Benki ya CRDB ilikuwa moja ya wadhamini wa mchezo wa mashindano hayo yaliyofanyika wiki iliyopita katika viwanja vya Gymkhana, Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Simbu ashika nafasi ya saba Marathon Olimpiki

**Na Mwandishi Wetu**

NDOTO ya Tanzania kuibuka na medali katika mashindano ya Olimpiki Tokyo, Japan, imezidi kudidimia baada ya mwanariadha tegemeo, Alphonce Felix Simbu, kumaliza katika nafasi ya saba kwenye mbio za Marathon juzi nchini humo.

Simbu alitumia muda wa saa 2:11:35 akishindwa kufua dafu kwa mshindi wa Medali ya Dhahabu ya mbio hizo, Mkenya Eliud Kipchoge aliyeongoza kwa kutumia muda wa saa 2:08:38.

Kwa ushindi huo Kipchoge ametetea vema taji lake la marathon na kuwa mwanariadha wa kwanza tangu mwaka 1980 kutwaa mfululizo wa Medali za Dhahabu ya Marathon kwenye Olimpiki na wa tatu kushinda mfululizo katika michezo hiyo.

Akipewa hadhi ya Mwanamarathon bora wa muda wote, mkimbiaji huyo mwenye umri wa miaka 36, alimaliza dakika moja na sekunde 20 kabla ya Mholanzi Abdi Nageeye aliyetwaa Medali ya Fedha, wakati Mbelgiji Bashir Abdi alimshinda Mkenya mwingine, Lawrence Cherono na kuibuka na Medali ya Shaba.

Wanariadha wengine waliomaliza 10-bora katika mbio hizo kwa upande wa wanaume ni Ayad Lamdassem wa Hispania aliyeshika nafasi ya tano, Suguru Osako (Japan) nafasi ya sita, Galen Rupp (Marekani) nafasi ya nane, Othmane El Goumri (Morocco) nafasi ya tisa na Koen Naert wa Ubelgiji aliyefunga hesabu kwenye 10-bora hiyo.

Wanariadha wengine wa Tanzania walioshiriki Olimpiki ya Tokyo ni Gabriel Gerald Geay, ambaye hakumaliza baada ya kuumia na Failuna Abdi Matanga akishika nafasi ya 24 upande wa wanawake.

Ni takribani miaka 41 sasa tangu Tanzania ilipotwaa kwa mara ya kwanza medali na ya mwisho katika michezo ya Olimpiki - mwaka 1980 jijini Moscow, Urusi kupitia kwa wanariadha Suleiman Nyambui Mujaya mita 5000 na Filbert Bayi Sanka mita 3000 wote wakishinda Medali ya Fedha baada ya kumaliza nafasi ya pili.

## Azam, KMKM zapania ubingwa Kagame CUP

**Na Saada Akida**

TIMU mbili za Tanzania, Azam FC (Tanzania Bara na KMKM (Visiwani), zimefanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano ya Kombe la Kagame ambayo inatarajiwa kuendelea kesho katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Azam FC, walioupata dhidi ya KMKM kwenye mchezo wa hatua ya makundi ya michuano hiyo unazifanya timu hizo mbili zote kutinga hatua ya nusu fainali.

Kwa matokeo hayo, sasa katika hatua ya nusu fainali timu hizo mbili kutoka Tanzania zitacheza nusu fainali zote zikitokea Kundi B.

Nusu fainali ya kwanza itaikutanisha Express FC ya Uganda dhidi ya KMKM kesho wakati Azam FC wakishuka dimbani Jumatano dhidi ya Nyasa Big Bullets ya Malawi.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanafanikiwa kubakisha kombe hilo nyumbani huku Kocha wa Mkuu wa KMKM, Ali Vua Shein, akisema licha ya ushindani mkubwa uliopo katika michuano hiyo wanahitaji kuendelea kufanya vizuri na kusonga mbele kucheza fainali.

## Geita Gold yanasa jembe JKT Tanzania

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Geita Gold ambayo imepanda Ligi Kuu msimu huu, imeanza kujiimarisha kwa kumsajili kiungo mkabaji, Kelvin Nashon kutoka JKT Tanzania ambayo tayari imeshuka daraja.

Nashon ametambulishwa kwenye mtandao rasmi wa kijamii wa klabu ya Geita Gold ukiandika "Karibu Kelvin Nashon," huku picha yake ikitawala kwenye ukurasa huo.

Kelvin ni mchezaji wa muda mrefu wa timu hiyo tangu ikiitwa, JKT Ruvu.

Wakati Geita Gold ikimtambulisha mchezaji huyo, klabu ya Prisons imemsajili kipa namba moja wa Dodoma Jiji, Aron Kalambo.


Ikumbukwe kuwa kabla ya kwenda Dodoma Jiji ambako aliitumikia kwa msimu mmoja, kipa huyo alikuwa kwenye klabu hiyo ya Prisons.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo kwenye mtandao wake wa kijamii ilisema: "Uongozi wa Prisons umefanikiwa kupata saini ya aliyekuwa kipa namba moja wa Dodoma Jiji, Aron Kalambo ambaye ataitumikia klabu yetu kwa msimu ujao wa 2021/22."

# Michezo

Jumatatu Agosti 9, 2021

Nipashe

Lukaku, Chelsea sasa ni rasmi kimeeleweka

HABARI UK. 22

INAUMA KUONDOKA...



Lionel Messi akishindwa kujizuia kumwaga machozi wakati akiaga rasmi katika Uwanja wa Camp Nou kuachana na klabu hiyo jana. Messi ambaye ameshinda mataji 35 na klabu hiyo, alisema kwa uchungu "mwaka jana, sikutaka kubaki na nilisema; mwaka huu, nilitaka kubaki na hatukuweza." **PICHA: MTANDAO**

# IBENGE AIGUSA SIMBA PABAYA

●●●Awataka Wamorocco wamletee haraka Mugalu kuisuka RS Berkane, ni wakati...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI leo wachezaji wa Simba wakiripoti kambini tayari kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu, Kombe la FA na michuano ya kimataifa, Kocha Mkuu wa Klabu ya RS Berkane ya Morocco, Mkongomani Florent Ibenge, ni kama amewagusa mabingwa hao wa Tanzania Bara sehemu mbaya baada ya kutaka kuibomoa safu yao ya ushambuliaji.

Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana jana kutoka nchini humo, Ibenge ambaye alisaini mkataka na klabu hiyo ya Morocco Julai 5, mwaka huu baada ya kuachana na AS Vita ya DR Congo, ameutaka uongozi wa RS Berkane kuhakikisha inatuma ofa ya kumsajili mshambuliaji wa Simba, Chris Mugalu 'The Animal'.

Mshambuliaji huyo raia wa DR Congo amekua chaguo la kwanza katika kikosi cha Simba chini Kocha Didier Gomes, akimpiku Mrundi Meddie Kagere, ambaye misimu miwili iliyopita ukiacha huu uliomalizika wa 2020/21, alikuwa mfungaji bora mara mbili mfululizo.

Mugalu msimu uliomaliza wa 2020/21, amemaliza na mabao 15 moja nyuma ya mfungaji bora, mchezaji mwenza wa Simba, John Bocco, huku Kagere akimaliza na mabao 13.

Hivyo, Ibenge ambaye alitimkia RS Berkane akitokea AS Vita Club, anaamini kama usajili wa Mugalu aliyetimiza miaka 31 juzi Jumamosi, utafanikiwa, atakuwa na safu bora ya ushambuliaji kwenye kikosi chake.

Lakini Simba iliyomsajili Mugalu wakati wa dirisha la usajili la 2020/21 akitokea Power Dynamos FC ya Zambia, huweza ikawa vigumu kumuuza kwani tayari Mwekezaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa klabu hiyo, Mohamed "Mo" Dewji, ameshaweka dhamira yake ya kuendelea kukijenga kikosi hicho na si kukibomoa kwa sasa.

Mo alisema lengo lake ni kutaka kuona wanatwaa ubingwa wa Afrika kwa kushindana na klabu kubwa barani humu kusajili wachezaji wa kiwango cha juu.

Tayari winga wa Simba, Luis Miquissone, inaelezwa ni suala la muda tu kabla ya msimu huu kujiunga na mabingwa wa Afrika, Al Ahly ya Misri kwa dau la zaidi ya Sh. bilioni mbili huku kiungo Clatous Chama naye akihusishwa na FAR Rabat ya Morocco.

Kwa mujibu wa taarifa, aliyekuwa Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck ambaye kwa sasa anainoa FAR Rabat, ameitaka klabu hiyo kumsajili Chama.

Kwa sasa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Barbara Gonzalez, yupo nchini Morocco na Ijumaa alikutana na Sven, ingawa haijaelezwa lengo la ziara yake hiyo, licha ya kuwataka Wanasimba watarajie mambo mazuri katika ziara hiyo.

Simba imeshatangaza usajili wa wachezaji wawili tu hadi sasa, mmoja mzawa, ambaye ni mshambuliaji Yusuph Mhilu kutoka Kagera Sugar na kiungo Mmalawi Peter Banda.

Simba itaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya msimu uliomalizika kuishia robo fainali na kufanikiwa kuiwezesha Tanzania Bara kuingiza timu nne kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF.

Timu nyingine itakayoiwakilisha Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa ni Yanga wakati Azam FC na Biashara United zikibeba jukumu hilo kwa upande wa Kombe la Shirikisho Afrika.

# Diarra wa Mali asaini Yanga, Johora kutua

**Na Saada Akida**

SASA ni rasmi Klabu ya Yanga imefanikiwa kuinasa saini ya Kipa raia wa Mali, Djigui Diarra, baada ya jana kusaini mkataba wa miaka miwili na miamba hiyo iliyomaliza nafasi ya pili Ligi Kuu Bara na kucheza fainali ya Kombe la FA msimu uliomalizika wa 2020/21.

Ujio wa kipa huyo, inaelezwa ndiye atakuwa chaguo namba moja la Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, kwani amekuwa akimhitaji kwa ajili ya kuimarisha nafasi hiyo ambayo imekuwa haina kipa namba moja hadi sasa kutokana na Metacha Mnata na Farouk Shikalo kucheza kwa kupokezana.

Kwa mujibu wa mshauri wa Yanga, Senzo Mazingiza, wamedhamiria kuimarisha kikosi cha timu hiyo kwa kufanyia kazi mapendekezo ya kocha Nabi, ambaye anahitaji kuona nafasi ya kipa, washambuliaji na beki ya kati ikifanyiwa maboresho makubwa.

"Usajili bado unaendelea, kuna wachezaji wengine watatua ndani ya wiki hii, viongozi wako makini, tutarajie kuona maboresho mazuri ndani ya kikosi cha Yanga, kuna Khalid Aucho na wengine ikiwamo nafasi ya kipa pia," alisema Senzo.

Hata hivyo, inaelezwa kipa mwingine anayetarajiwa kujiunga na Yanga ni Mtanzania Eric Johora anayeichezea Aigle Noir ya Burundi.

Nipashe lilipomtafuta Johora kujua ukweli kuhusu tetesi hizo, alisema: "Ni kweli nipo kwenye mazungumzo na viongozi wa Yanga, mambo madogo ya mkataba yanakwamisha, hadi sasa sijasaini ila bado tunaendelea kuzungumza, nina imani tutafikia muafaka kila kitu kitakuwa wazi na lolote unaweza kusikia," alisema Johora.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >